# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja 0, la kwanza na la pili

Mfululizo wa B
Masomo ya kwanza hadi ya sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya “Wakati na Biblia/Bibletime”, “Maisha Mapya/New Life” na “Wakusanyaji/Gleaners” kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) zaidi ya miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wameendelea kuchukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wa kufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa ili kutumika nyumbani au kwenye vikundi kama vile kutoka kwenye makanisani na kwenye shule. Masomo haya yameandaliwa kwa kuzingatia vyema mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na unaomruhusu mwanafunzi kuyatumia hadi atakapotimiza umri wa miaka 20. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (Daraja 0) ambao wana umri wa chini ya miaka mitano, miaka mitano hadi saba (Daraja la 1), miaka nane hadi kumi (Daraja la Pili), miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu (Daraja la Tatu) na miaka kumi na minne hadi kumi na sita (Daraja la Nne). Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 4). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongozo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwaajili ya mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES


**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo kwa Walimu umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo kwa Walimu katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya Daraja 0, Daraja la kwanza na Daraja la pili kwa watoto wenye umri kutoka chekechea hadi wastani miaka 10. Masomo ya Daraja 0 hayajajapishwa ila yanaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti ya BES.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

Tutashukuru kama tutapata mrejesho kuhusu matumizi ya Miongozo ya Waalimu na kwa ajili ya vitabu vya Wakati na Biblia na mrejesho huo utumwe kwa stephen.gillham@besweb.com.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Mwongozo huu wa Walimu siyu shinikizo ambao hauwapi walimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri** – Walimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadiri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza** – Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza jambo linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Walimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi** – Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha** – Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba walimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze** – Kuna Mstari Muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari Muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha** – Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu walimu kuwepo na kuwasaidia watoto ili wasichukulie masomo haya kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka** – Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha** – Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadiri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadiri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwisho wa Mwongozo wa Walimu kuna viambatisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha tofauti na zinazofaa kwa kila habari kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
    1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
    2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi 10
    3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
    4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi 10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/Chini ya miaka mitano) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

## B1 Habari ya Kwanza

**Mariamu na Yusufu hekaluni - Habari hii inahusu kusema "Asante" kwa Mungu kwa ajili ya Mwanawe**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Mtoto Yesu alizaliwa awe Wokovu wa Mungu.<br>• Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kumtoa Mwanawe kuwa Mwokozi wetu.<br><br>Mstari Muhimu: Luka 2: 30<br>Neno la Biblia: Luka 2: 22-38</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Zungumzia kuhusu kupokea zawadi; ikiwezekana andaa zawadi moja au mbili zilizofungwa vizuri kwa ajili ya kutolewa ili kusema "Asante" kudhihirishwa kimatendo. Waulize watoto wataje kitu walichokipokea kikawafanya wafurahie sana. Sisitiza umuhimu wa kusema "Asante" mtu anapopokea zawadi yoyote, hata kama ni ndogo.<br>Katika habari hii ya leo tunakutana na watu waliokuwa na shukrani kwa ajili ya zawadi kuu ya Mungu, yaani Bwana Yesu.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Leo ilikuwa siku muhimu sana kwa Mariamu na Yusufu. Walimleta mtoto Yesu hekaluni huko Yerusalemu ili kumshukuru Mungu (Luka 2:22-24).<br>• Wakiwa huko, mzee mmoja kwa jina lake Simeoni aliwasogelea. Mtu huyu aliujua mpango wa Mungu wa kumtuma Mwokozi – Kwa hakika alipewa ahadi ya ajabu kwamba hatakufa mpaka amemuona Bwana Yesu. Roho Mtakatifu alimwongoza Simeoni kukutana na Mariamu na Yusufu siku hiyo hiyo! Simeoni alifahamu tofauti kubwa ambayo Mtoto huyu wa kipekee angeileta ulimwenguni kote. Alifahamu jinsi Yesu alivyokuwa zawadi ya thamani. (Tafakari hisia alizokuwa nazo Simeoni alipombeba Mtoto Yule mikononi mwake na kumshukuru Mungu). (Luka 2:25-35)<br>• Bibi mmoja kwa jina lake Ana pia aliwakuta Mariamu na Yusufu wakiwa na Mtoto Yesu. Yeye pia alimshukuru Mungu kwa ajili ya Yesu. Baada ya hapo alimwambia kila aliyekutana naye kumhusu Yesu (Luka 2:36-38). Tunapaswa kupenda kuwashirikisha wengine Habari Njema kuhusu kuzaliwa kwa Yesu kama alivyofanya Ana!<br><br>Ni watu wangapi walisema "Asante" wakiwa hekaluni? Wahesabu na kuwataja majina.<br>Ni muhimu kwetu pia kumshukuru Mungu kwa ajili ya Bwana Yesu. Katika kipindi cha maisha ya Simeoni, kila wakati alitazamia siku atakapozaliwa Yesu.Tunaweza kukumbuka mambo ya hapo awali na kushukuru kwa ajili ya kuzaliwa kwa Yesu na kufanyika Mwokozi wetu kwa kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Watie moyo watoto watambue thamani ya zawadi nzuri ya Mungu ukilinganisha na zawadi za vitu na mhamasishe kila mmoja amshukuru Mungu kibinafsi kwa ajili ya Bwana Yesu na yote aliyotutendea.<br><br>Kamilisha somo la Wakati na Biblia.<br><br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kutoa shukrani hekaluni/ Mariamu na Yusufu hekaluni.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. Luka 2: 30.<br>Elezea kwamba maneno haya ni sehemu ya sala ya Simeoni yakusema "Asante". Jambo ambalo Bwana Yesu anatupa anapoziondoa dhambi zetu ni wokovu.</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Hekalu lilikuwa wapi?<br>• Kwa nini Mariamu na Yusufu walikuwa huko pamoja na Yesu?<br>• Ni mzee gani alikuja kwao?<br>• Simeoni alipewa ahadi gani?<br>• Bibi aliyetoa shukurani kwa ajili ya Yesu anaitwa nani?<br>• Ana alifanya nini baada ya kumuona mtoto Yesu?<br>• Tunajifunza nini kutokana na mfano wa Simeoni na Ana?<br>• Ni katika kitabu gani cha Biblia tunasoma habari za Simeoni na Ana?</td></tr>
</table>

## B1 Habari ya Pili

**Kukulia Nazareti – Habari hii inahusu Yesu akikua kama kijana.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu akiwa mvulana, alidhihirisha kuwa alikuwa Mwana wa Mungu.<br>• Ni muhimu kufuata mfano wa Yesu na kuwa mtiifu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 40 – (Au Waefeso 6: 1)***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 2: 39-52*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumzia kuhusu kupotea njia au kutenganishwa na wazazi wako. Ilitokeaje au ilitokea wapi? Elekeza mjadala katika namna ambavyo wazazi wangehisi?<br><u>Au</u><br>Kama itafaa, zungumza kuhusu uzoefu wa kusafiri mbali na nyumbani na msisimko wote ulioambatana na safari hiyo. Elezea kwamba katika habari ya leo Mariamu na Yusufu walimpeleka Yesu kwenye tukio maalum mbali na nyumbani. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikuwa Yerusalemu pamoja na wazazi Wake kusherehekea Sikukuu ya Pasaka. *(Kwa watoto wakubwa wenye maarifa ya Biblia, eleza maana ya tukio hili.) Washirikishe watoto kutafakari kuhusu umbali wake (umbali wa maili 70 kutoka Yerusalemu hadi Nazareti) kwa kulinganisha na umbali wa eneo wanakoishi na uelezee jinsi walivyotembea kwa miguu. Jadili jinsi safari hii ilivyomfurahisha Yesu aliyekuwa na umri wa miaka 12 – umati wa watu, marafiki zake, majengo na fursa ya kuwepo Hekaluni ambapo waalimu walizungumza kuhusu Mungu Baba Yake.* ***(Luka 2: 42)***<br>• Baada ya siku ya kwanza ya safari ya kurudi nyumbani, Mariamu na Yusufu waligundua kuwa Yesu hakuwa pamoja nao! Chunguza hisia zao na utafakari jinsi gani walimtafuta Yesu katika ule umati na kisha kuamua kurudi Yerusalemu. ***(Luka 2: 43-45)***.<br>• Baada ya siku tatu walimkuta Yesu akiwa Hekaluni amekaa katikati ya waalimu. *Elezea faraja yao na kuihusisha na Utangulizi.* Alipokuwa akiwasikiliza na kuwauliza maswali, waalimu walishangazwa na ufahamu wake kuhusu Mungu. Mariamu na Yusufu nao pia walishangazwa! Linganisha mazungumzo kati ya Mariamu na Yesu na elezea kuwa hata sasa akiwa mvulana wa umri mdogo, Yesu alikuwa akifanya kazi nyumbani kwa Baba Yake (Hekaluni). Ilikuwa vigumu kwa Mariamu na Yusufu kuelewa vizuri alichokuwa anasema Yesu ***(Luka 2: 46-50).***<br>• Baada ya hili, Yesu alirudi Nazareti pamoja na Mariamu na Yusufu. Yesu alikuwa mtiifu kwa wazazi wake kwa kila namna, akiwapendeza na vile vile kumpendeza Mungu, Baba Yake. *Biblia inatuambia inatupasa kuwa watiifu kwa wazazi wetu.* ***(Waefeso 6:1)*** *kwa kufanya tunavyoambiwa; tunafuata mfano wa Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kukulia Nazareti. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. ***Luka 2:40 – (Au Waefeso 6:1)***<br>Eleza kwamba inataja njia tofauti ambazo Yesu alikua. Tunaweza kukua katika njia hizi pia – zaidi ya yote, Mungu anatutaka tukue na kuwa watu wanaompenda na kumtumikia. |
| **KUMBUKA** | <u>**Tumia maelezo haya ambayo ni ya kweli/siyo kweli kwa ajili ya zoezi.**</u><br>• Sikukuu ya Pasaka ilikuwa Yerusalemu.<br>• Yesu alikuwa na umri wa miaka 10 katika habari hii.<br>• Mariamu na Yusufu walimuona Yesu baada ya siku moja.<br>• Yesu alikuwa katika nyumba ya jamaa zake.<br>• Mariamu alimwambia Yesu kwamba walikuwa na wasiwasi.<br>• Yesu alikuwa akifanya kazi ya Baba Yake.<br>• Mungu ni Baba wa Bwana Yesu.<br>• Yesu alirudi Nazareti na kuwatii Mariamu na Yusufu. |

**<u>B1 Habari ya Tatu</u>**

**Kubatizwa katika Mto Yordani – Habari hii inahusu Yesu kubatizwa na Yohana.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Maisha ya Yesu yalikuwa hayana dhambi na siku zote alimpendeza Baba Yake.<br>• Sisi ni wenye dhambi na tunahitaji kutubu dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 3: 22***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 3: 1-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu watu wanaokusanya umati wa watu - kwa mfano, mgeni wa kifalme, rais, waziri mkuu, mtu anayeuza bidhaa sokoni, msanii wa mtaani. Kila mtu anataka kuona kinachotokea au kusikia kinachosemwa. Haitofautiana na Yohana alipoanza kuhubiri kando ya Mto Yordani. Umati ulikusanyika kusikia kitu ambacho alikuwa akisema huyu mtu mwenye mwonekano wa tofauti aliyeishi nyikani. ***(Mathayo 3: 4)*** |
| **FUNDISHA** | • Yohana alikuwa nabii. Hii ina maana kwamba Yohana alipewa ujumbe muhimu kutoka kwa Mungu. Aliwaambia watu kwamba walikuwa wenye dhambi na walipaswa kujutia mabaya waliyoyafanya na kuacha kuyatenda. *(Hii inaitwa toba)*. Baada ya hapo walibatizwa kwa kuzamishwa katika Mto Yordani. Hili lilidhihirisha kwamba waliazimia kwa dhati kubadili njia zao ***(Luka 3: 2,3,7)****. Kama watoto wamewahi kushuhudia ubatizo wa Kikristo, unganisha hili na uzoefu wao. Eleza kuwa sote tunahitaji kujutia (kutubu) makosa tuliyotenda.*<br>• Watu hao bado hawakuwa na uhakika kuwa Yohana alikuwa nani. Je ndiye Yule ambaye Mungu aliahidi kuwa atamtuma? Yohana alieleza kwamba kuna mwingine mwenye nguvu zaidi yake atakayekuja. ***(Luka 3: 15 &16)***. Mtu huyo anaweza kuwa ni nani?<br>• Basi siku moja Bwana Yesu alijitokeza pamoja na watu wengine naye pia akabatizwa. Ni nini Yesu hakuhitaji kukifanya kabla hajabatizwa? *Jadili ukweli wa suala hili kuwa Yesu alikuwa wa tofauti na wengine wote (na sisi) kwa sababu hakuwa na dhambi na hakuhitaji kutubu.* Lakini Yesu alitaka kuonesha kuwa alikuwa mwanadamu kama sisi, na pia kutenda kile ambacho Mungu alisema. Baada ya ubatizo wa Yesu, jambo la ajabu likatokea, Mungu Alinena kutoka mbinguni, akisema kuwa Amependezwa sana na Mwanawe, na hapo Roho Mtakatifu akashuka kama hua juu Yake. ***(Luka 3: 21, 22)****. Ni kwa nini Mungu alipendezwa sana na Bwana Yesu?*<br>• *Hatuwezi kumpendeza Mungu kwa namna ambayo Yesu Alifanya. Lakini Mungu Anapendezwa tunapojutia dhambi zetu (kutubu) na kuamua kuishi kwa ajili Yake.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kujiandaa kwa ajili ya Yesu / Kubatizwa katika Mto Yordani. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. ***Luka 3: 22 (Sehemu b).***<br>Uliza maswali mepesi ili kujua kama watoto wameelewa muktadha wake. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Yohana alikuwa anahubiri wapi?<br>• Yohana alipata ujumbe wake kutoka wapi?<br>• Yohana aliwaambia watu “watubu.” Je, hii ina maana gani?<br>• Yohana aliwafanyia nini watu baada ya kutubu?<br>• Yohana alimuelezeaje mtu ambaye atakuja baada yake?<br>• Yesu alimtaka Yohana afanye nini?<br>• Kiasi gani ubatizo wa Yesu ulikuwa tofauti na wa wengine?<br>• Ni kwa namna gani tunaweza kumpendeza Mungu? |

## <u>B1 Habari ya Nne</u>

**Kujaribiwa nyikani – Habari hii inahusu kusema “Hapana” kwa maovu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Bwana Yesu hakuwahi kutenda dhambi.<br>• Anao uwezo wa kutusaidia tunapojaribiwa kutenda mabaya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 4: 8***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 4: 1-13*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wape watoto mfano unaoendana na hali zao za jinsi wanavyoweza kujaribiwa. (tazama mfano mwanzoni mwa somo la Daraja la 2). Zungumzia ni kwa jinsi gani wataweza kuyashinda majaribu katika uhalisia. Leo tutajifunzi ni nini Yesu alifanya alipojaribiwa. |
| **FUNDISHA** | • Baada ya ubatizo wa Yesu, Roho Mtakatifu Alimwongoza kwenda Nyikani/ Jangwani. *Jadili hali ilivyokuwa jangwani kwa siku 40 – joto, ukame, upweke... Tafuta mfano mzuri wa kulinganisha ili kuwasaidia watoto kufahamu jinsi siku 40 zilivyo nyingi.* ***(Luka 4: 1-2)***<br>• Yesu hakula chochote kwa muda mrefu, kwa hiyo aliona njaa sana! Zaidi ya yote, bila shaka Yesu alihitaji chakula. *Nukuu pendekezo ambalo ibilisi alimletea Yesu. Unaona jinsi hii ilivyokuwa ni njia rahisi ya kupata mkate!* Lakini Yesu alijibu kwa kutumia mstari kutoka katika Neno la Mungu ambalo linasema kuwa jaribu la ibilisi halikuwa sahihi. ***(Luka 4: 3-4)***<br>• Ibilisi alirudi tena kwa Yesu na kumpandisha kwenye mlima mrefu na kumuonesha milki zote za ulimwengu. Akasema kwamba kama Yesu angesujudu mbele yake, angelimpa milki zote hizo. Yesu akajibu “imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako na umwabudu Yeye peke yake’’. Kwa mara ya pili, Yesu alitumia maneno ya Biblia kumuonesha ibilisi jinsi ambavyo wazo lake halikuwa sahihi. ***(Luka 4: 5-8)***<br>• Hatimaye, ibilisi alimwongoza Yesu mpaka Yerusalemu, akamweka juu ya kinara cha hekalu. Akamwambia ikiwa ni Mwana wa Mungu, ajitupe chini na hutaumia. Alikuwa anamjaribu Yesu ajivunie nguvu Zake. Lakini Yesu alijua hili pia litakuwa ni kosa na akamwambia ibilisi tena akitumia maneno kutoka katika Biblia. Kwa hatua hii ibilisi akamwacha Yesu. ***(Luka 4: 9-13)***. *Unadhani kwa nini ibilisi aliondoka? Je alikuwa amefanikiwa? Ni kwa namna gani Yesu aliweza kuyashinda majaribu?*<br>• *Hitimisha kwa kubainisha kuwa Bwana Yesu hakuwahi kutenda dhambi. Yesu ni Mwenye Nguvu kuliko ibilisi. Alitumia Neno la Mungu kumuonesha ibilisi kuwa Alimtii Mungu Baba Yake. Ikiwa sisi ni wa Bwana Yesu, Atatusaidia kukataa mambo mabaya. Ikiwa tunalijua Neno la Mungu kama Bwana Yesu alivyolijua, tutaweza kulitumia ili litupe nguvu ya kufanya mambo sahihi.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kujaribiwa nyikani / Yesu Akutana na Yohana. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea ***Luka 4: 8.***<br>Dadisi ujue kama watoto wanakumbuka muktadha wa mstari huu. Nani aliusema? Ulimlenga nani? Ni kwa nini Yesu aliyatumia haya maneno? |
| **KUMBUKA** | Badala ya jaribio, ni bora “kuchemsha bongo” kwa yale yote ambayo watoto wamejifunza kumhusu Bwana Yesu katika B1. Mwalimu anaweza kuyaandika mawazo (andika sentensi fupi au maelezo mafupi) kwenye bango mgeuzo. Watoto wa umri mkubwa wanaweza kuanza kufanya kazi katika vikundi vidogo na kisha kuleta mrejesho kwa mwalimu. |

## B2 Habari ya Kwanza

**Yesu Ageuza maji kuwa divai – Habari hii inahusu Yesu akiwa kwenye karamu ya harusi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alitenda muujiza huu wa kwanza kwa sababu ni Mwana wa Mungu.<br>• Inatupasa kumtii kama watumishi katika habari hii walivyomtii.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 2:5***<br>**Neno la Biblia:** ***Yohana 2:1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu kinachotekea harusini katika tamaduni zenu. Wape nafasi watoto washirikishe uzoefu wao. Kama itawezekana uwe na picha chache. Je, ingekuwaje kama jambo fulani harusini halikufanyika kama ilivyopangwa? Pendekeza mfano mmoja au miwili.<br>Katika habari ya leo, Bwana Yesu, wanafunzi Wake, na mama Yake, yaani Mariamu, walialikwa kwenye harusi mahali panapoitwa Kana. ***(Yohana 2:1-2)***. Hebu tuone kilichotokea. |
| **FUNDISHA** | • *Elezea tukio – Bibi harusi na bwana harusi, wageni, wakizungumza na kucheka, vyakula vitamu na vinywaji, kila mtu akifurahia harusi. Walakini Mariamu akatambua kuwa kuna kitu hakikuwa sawa – divai ilikuwa imekwisha! Je, bibi harusi na bwana harusi walijisikiaje?* Mariamu alijua cha kufanya. Mara moja akamwambia Yesu. Eleza kuwa Yesu ndiye Mtu bora zaidi kupelekewa tatizo lolote lile. Tunaweza kumuomba Yesu. Mariamu akawageukia watumishi na kusema, “Lolote atakalowaambia, fanyeni”. Mariamu alijua kuwa Yesu Ataweza kuwasaidia. Alimwamini Yesu kikamilifu ***(Yohana 2:3-5)***.<br>• *Eleza kuwa ndani ya chumba palikuwepo mabalasi sita ya mawe (kila moja lapata kadiri ya mita moja urefu) mabalasi ambayo kuna uwezekano kwamba yalitumiwa kubeba maji ya kupikia au kunawia mikono.* Yesu aliwaambia watumishi, wayajalize mabalasi yale maji hadi juu na kisha wachote ili kumpelekea mkuu wa meza.T*afakari ukweli kwamba yawezekana hili jambo lilikuwa geni kufanya...* Hakika haya yalikuwa maji tu? Lakini walitii na kwa mshangao, hayakuwa maji tena. Ilikuwa ni divai! Kwa kweli, wote walikubaliana ya kuwa ilikuwa divai NJEMA, zaidi ya waliyokunywa awali. ***(Yohana 2: 6-10)*** *Siku zote Bwana Yesu hutoa kilicho chema!*<br>• *Eleza kwamba huu ulikuwa muujiza. Hakuna mwingine angeliweza kutenda kile Yesu alichokitenda. Alitenda hili kwa sababu Yeye ni Mwana wa Mungu, Muumbaji wa vitu vyote.*<br>• *Ilikuwa muhimu sana kwamba watumishi walimtii Yesu. Waulize watoto kutafakari nini kingetokea kama wasingetii. Zungumzia tatizo tulilo nalo – dhambi zetu. Bwana Yesu ana suluhisho la tatizo letu kwa sababu Alikufa msalabani ili kuchukua adhabu ya dhambi zetu. Lakini ni pale tu tunapoweka tumaini letu Kwake kuwa Anaweza kutenda muujiza katika maisha yetu na kutusamehe dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu ageuza maji kuwa divai. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu.***Yohana 2: 5***. Toa muktadha wa habari hiyo. Hakikisha watoto wanajua “Bwana” anayezungumziwa ni nani. Watoto wadogo wanaweza kujifunza sehemu ya pili ya mstari huo. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Harusi ilikuwa wapi?<br>• Taja baadhi ya wageni waliokuwepo harusini.<br>• Ni nani aliyewaambia watumishi wamsikilize Yesu?<br>• Yesu aliwaambia watumishi wafanye nini?<br>• Kulikuwa na mabalasi mangapi?<br>• Kulitokea nini watumishi walipochota maji yaliyokuwa ndani ya mabalasi?<br>• Kitu gani kilikubaliwa na kila mtu?<br>• Kwa nini Yesu aliweza kutenda muujiza huu?<br>• Kuna tatizo gani katika maisha yetu?<br>• Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa watumishi? |

## B2 Habari ya Pili
**Yesu Amponya kijana mgonjwa – Habari hii inahusu nguvu za Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu Alikuwa na nguvu za kuponya kwa sababu ni Mwana wa Mungu.<br>• Yesu Anatutaka tumtumaini Yeye kama diwani alivyofanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 4: 50***<br>**Neno la Biblia:** ***Yohana 4: 46-54*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Rejelea habari ya wiki iliyopita. Ni nini kilichotokea harusini? Kilitokea wapi? Zungumzia jinsi taarifa za muujiza huu zilivyoenea katika eneo la Kana na kwengineko. Yule diwani katika habari ya leo bila shaka alizisikia taarifa za mambo yote ambayo Yesu alikuwa akiyatenda. |
| **FUNDISHA** | • Punde baadaye Yesu alirudi Kana. Katika mji wa karibu wa Kapernaumu, mtu muhimu (diwani) alisikia kwamba Yesu amekuja Kana. *Alijiuliza kama Yesu angeliweza tu kumsaidia!* Kwa maana mwanawe alikuwa mgonjwa sana. Yule diwani aliwaza kwamba kama Yesu angekuja nyumbani kwake, angemponya mwanawe. ***(Yohana 4: 47)*** *Kwa wale watoto wa daraja la 2 ikiwezekana uwaoneshe ramani inayoonesha miji hii miwili.*<br>• Yule diwani alisafiri safari ya maili ishirini ili kukutana na Yesu. *Hebu tafakari alivyojihisi – kuchoka, wasiwasi, kukata tamaa. Alimsihi Yesu afuatane naye hadi nyumbani kwake. Alipomwambia kuhusu mwanawe, Yesu akamwambia enenda mwanao yu hai. Yesu hakuondoka naye! Tafakari ni kwa jinsi gani angeliweza kuhisi na kisha eleza kwamba alisadiki lile neno aliloambiwa na Yesu. Alikuwa na imani kubwa kwa Yesu kiasi kwamba alijua kuwa haikumlazimu Yesu kusafiri maili ishirini ili kumponya mwanawe.* ***(Yohana 4: 47-50)*** *Eleza ya kwamba Yesu anataka aina hii ya Imani kutoka kwetu. Hatuwezi kumuona Yesu au kumsikia akizungumza kwa sauti kubwa lakini Ameahidi katika Neno Lake, yaani Biblia, ya kuwa Anatupenda na Anataka kutusamehe.*<br>• Mtu huyu alipokuwa safarini kuelekea nyumbani, watumishi wake walimlaki wakiwa na habari njema. *Waulize watoto kusema habari hiyo njema ilikuwa ipi.* Ndiyo! Mwanawe alikuwa amepona... na alipouliza ni muda gani jambo hilo lilitokea, aligundua kuwa ni saa ile ile aliyoambiwa na Yesu, Mwanao yu hai. Unadhani familia nzima ilijawa furaha kiasi gani! Wote walikuwa na uhakika kwamba Yesu alikuwa kama alivyodai kuwa – Mwana wa Mungu. ***(Yohana 4: 51-53)***<br>• Sisi pia tunapaswa kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu. Yesu Anatutaka tudhihirishe tumaini letu kwake.Hapo ndipo sisi pia tutakuwa na furaha ya kweli.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu amponya kijana mgonjwa. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, pale inapolazimu, Mstari Muhimu. ***Yohana 4:50***. Sisitiza maana ya kumuamini mtu kwa neno lake analolisema. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Tatizo la diwani lilikuwa nini?<br>• Alimkuta Yesu wapi?<br>• Alitakiwa kusafiri umbali gani?<br>• Yesu alimwambia afanye nini?<br>• Ni nani walikutana naye alipokuwa akirudi nyumbani?<br>• Walikuwa na habari gani njema?<br>• Ni lini mtoto alipona?<br>• Jaza neno katika nafasi iliyo wazi – “Diwani ________ Yesu kikamilifu”. |

## B2 Habari ya Tatu

**Yesu na Bartimayo – Habari hii inahusu uponyaji wa mtu kipofu ambaye hatimaye alimfuata Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Bwana Yesu alitaka kumsaidia Bartimayo na alikuwa na nguvu za kubadilisha maisha yake.<br>• Yesu anataka kubadilisha maisha yetu kwa kuziondoa dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 10: 52***<br>**Neno la Biblia:** ***Marko 10: 46-52*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumzia kuhusu zawadi ya ajabu ya kupata kuona – kuweza kuona rangi, kufurahia sehemu mbalimbali, kuwatambua watu, kusoma vitabu, kufurahia michezo, kutazama runinga n.k. Kwa umakini na kwa kujali hali ya Wanafunzi wote darasani, jadili maisha yangekuwaje kwa mtu kipofu katika jamii unapoishi. Eleza kwamba katika wakati wa Yesu, maisha yangekuwa magumu sana kwa mtu kipofu. |
| **FUNDISHA** | • Bartimayo alikuwa mtu kipofu aliyeishi Yeriko. Kwake yeye, siku zote zilifanana – kuombaomba kando ya njia ili kujikimu mahitaji yake. Lakini siku ya leo ilikuwa ya tofauti. *Fafanua zile kelele, mkutano mkubwa na Bartimayo kugundua kwamba Yesu alikuwa akipita njia hiyo.* Ghafla Bartimayo akajawa na furaha! Alisikia kuhusu mambo Yesu aliyoyatenda. *Je unadhani ni kitu gani alitaka Yesu amtendee?* Bartimayo alianza kupaaza sauti yake kwa nguvu zake zote, akimsihi Yesu amsaidie. Na wengi wakamkemea ili anyamaze lakini alizidi kupaza sauti yake! ***(Marko 10: 46-48)*** *Elezea kwamba Bartimayo alikuwa akifanya jambo sahihi kwa sababu ni Yesu pekee ambaye angeweza kumfanya aweze kuona. Bwana Yesu ndiye pekee Awezaye kutusamehe dhambi zetu. Kama jinsi Bartimayo alivyohitaji kukutana na Bwana Yesu Sisi nasi twahitaji msaada Wake pia.*<br>• Kwa hatua hiyo, Yesu akasimama na kumwambia mtu amwite Bartimayo aje Kwake. *Elezea jinsi Bartimayo alivyoitikia. Je, Bartimayo alikuwa akijihisi vipi wakati huu?* Yesu alimuuliza anachokitaka naye akajibu kuwa alitaka kuweza kuona. Yesu akamwambia, enenda zako, Imani yako imekuponya. Mara Bartimayo akaweza kuona! *Waulize watoto watoe maoni yao kwamba wanadhani aliona vitu gani vimemzunguka. Elezea hisia zake na mwitikio wake katika kumfuata Yesu njiani.* ***(Marko 10: 49-52)***<br>• *Bartimayo kamwe hangesahau siku ile alipokutana na Yesu. Yesu alimtendea muujiza na maisha yake yakabadilishwa! Elezea kuwa Bwana Yesu anataka kututendea muujiza mkubwa zaidi kwa kubadilisha maisha yetu ya ndani na kuziondoa dhambi zetu. Tukija kwake Yesu na kumwamini tutapata furaha ya kweli kama vile Bartimayo alivyoipata.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu na Bartimayo kipofu / Yesu na kipofu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na eleza, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Marko 10: 52***. Eleza kwamba "Imani" ya Bartimayo ilikuwa ni tumaini lake kwa Bwana Yesu. Alijua kuwa Yesu alikuwa anazo nguvu za kumrejeshea kuona kwake. Yesu anataka sisi tuwe na imani kwake. Mstari mbadala wa Biblia unaweza kuwa ***Yohana 8: 12 - sehemu b*** |
| **KUMBUKA** | Jibu kweli au si kweli katika sentensi za jaribio hili.<br>• Bartimayo alikuwa Kana.<br>• Alikuwa kipofu.<br>• Hakuweza kuzungumza.<br>• Palikuwa na watu wengi waliotaka kumuona Yesu.<br>• Bartimayo alikaa kimya watu walipomwambia afanye hivyo.<br>• Yesu alijifanya kama hamsikii.<br>• Bartimayo alisimama na kuja kwa Yesu.<br>• Umati wa watu ulimzuia kuja kwa Yesu.<br>• Bartimayo aliendelea kuombaomba hata baada ya kukutana na Yesu.<br>• Bwana Yesu Anaweza kutenda muujiza kwa ajili ya kila mmoja wetu. |

## B2 Habari ya Nne

**Yesu Awaponya watu kumi wenye ukoma – Habari hii inahusu kusema "Asante Kwa Yesu".**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Watu wenye ukoma walimtii Yesu na wakaponywa.<br>• Bwana Yesu Anataka tumshukuru kwa wema Wake kwetu sisi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 107:21***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 17: 11-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu kuwa mtu mwenye shukurani. Waulize watoto kufikiri vitu ambavyo wanaweza kushukuru kwa kuvipata kila siku (mfano. chakula, maji, makazi, afya, familia, shule) na kuviorodhesha vitu vyote watakavyovitaja. Eleza kwamba Mungu ndiye mpaji wa vitu vyote vyema tunavyovifurahia na anza kwa maombi ya shukurani, ukiwakumbuka wale wote wenye uhitaji. |
| **FUNDISHA** | • Habari ya leo ni kuhusu watu kumi waliokuwa na maisha magumu. *Eleza jinsi gani ukoma uliwaathiri. – Tazama utangulizi wa habari kwenye Wakati na Biblia daraja la 1 au 2.*<br>• Siku moja, jambo la kuvutia lilitokea. Yesu alitembelea eneo waliloishi. Ingawaje hakuna mtu aliruhusiwa kumkaribia, waliweza kumuona kwa mbali na walijua kuwa Yesu angeweza kuwasaidia. Wakapaaza sauti kwa pamoja kadiri walivyoweza, "Ee Yesu, Bwana mkubwa, uturehemu!" ***(Luka 17: 11-13)***<br>• Yesu aliwasikia na kuwaambia, "Enendeni, mkajioneshe kwa makuhani." *Eleza kwamba Torati ilisema kuwa yeyote aliyeponywa ukoma alipaswa kwenda kwa kuhani kuthibitisha kuwa ni kweli.* Watu wale walitambua kwamba Yesu alikuwa anawaponya kwa hiyo mara moja walimtii Yesu na kuondoka.Ikawa walipokuwa wakienda ghafla ukoma ukatoweka! Yesu alikuwa amewaponya. *Je, walijisikiaje?* ***(Luka 17: 14)*** *Walifanya jambo sahihi katika kumtii Yesu. Nasi pia tunahitaji kumtumaini na kumtii Yesu kama tunataka kupata baraka au mambo mema Aliyo nayo kwa ajili yetu.*<br>• Wale watu kumi walishangazwa na mabadiliko ya ajabu yaliyotokea lakini ni mmoja wao tu aliwaza kurudi ili aseme "asante". Alipokuwa akimtukuza Mungu kwa kile kilichotokea, alirudi upesi na alipomkuta Yesu akaanguka miguuni pake. *Eleza kwamba mtu huyu alikuwa tofauti kwa sababu alikuwa Msamaria na hakutoka katika nchi ile ambayo Yesu au wengine walitokea.* Yesu alipendezwa sana na mtu huyu kwa kuwa alikuwa mwenye shukurani na Alimsifia kwa kuonyesha imani alipotii. *Je, unafikiri Yesu Alihisi vipi kuhusu wale wengine tisa?* ***(Luka 17: 15-19)****. Unadhani ni nani aliyekuwa na furaha kuliko wote siku hiyo?*<br>• *Tunapaswa kuwa wenye shukurani kwa Mungu (wakumbushe watoto mambo yaliyo kwenye orodha yao) na pia kwa Bwana Yesu Aliyetoa maisha Yake ili dhambi zetu zisamehewe. Watie moyo watoto wafuate mfano mzuri wa mtu yule katika habari hii.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu awaponya watu kumi wenye ukoma. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na eleza, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Zaburi 107: 21.*** Eleza maneno yote magumu ambayo hayaeleweki – k.m kutokushindwa, matendo |
| **KUMBUKA** | Badala ya jaribio, watoto wanaweza kuchora picha huku kila mtoto akishiriki katika zoezi hilo kwa kuleta picha ya kitu anachotaka kumtolea Mungu shukurani. Watoto wengine wanaweza kupaka rangi maneno ASANTE MUNGU! wayaweke katikati ya hizo picha.<br><br>Kundi dogo la watoto wadogo wanaweza kutengeneza maumbo rahisi kumi kuwakilisha wenye ukoma 10.<br>1. Chukua kipande kipana cha karatasi na ukifanye kuwa na mikunjo kumi au kweye mtindo wa Concertina kwa Lugha ya Kiingereza yenye sehemu kumi.<br>2. Chora mchoro wa mtu sehemu ya juu ya karatasi au kwenye mkunjo wa juu na mikono yake iwe imenyooka hadi pembeni mwa mkunjo wa sehemu hiyo.<br>3. Kata ukizunguka umbo hilo la mtu kupitisha katika mikunjo yote kumi na utapata mnyororo wa maumbo 10 ya wenye ukoma. |

## B3 Habari ya Kwanza

**Kujifunza kutoka kwa Yesu – Habari inahusu kutenga muda ili kujifunza kutoka kwa Yesu.**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Kumsikiliza Yesu na kujifunza kutoka kwake ni jambo muhimu sana.<br>• Tunahitaji kumsikiliza Yesu kupitia kuisoma Biblia.<br><br>Mstari Muhimu: Luka 10: 42<br>Neno la Biblia: Luka 10: 38-42</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Chagua wazo moja:<br>• Zungumza kuhusu jinsi ambavyo mama yako angejiandaa kwa ajili ya kupata wageni nyumbani kwenu – kupika chakula n.k.<br>• Zungumza kuhusu hali mbalimbali ambazo ni muhimu kwa watoto – wakati ambapo ni muhimu kusikiliza – kujifunza ujuzi mpya, kupokea maelekezo...<br>• Ukiwa na kundi dogo mnaweza kucheza “mchezo wa kunong’onezana sikioni”. Hapa yule kiongozi anamnong’onezea ujumbe mtu wa kwanza ambaye naye atamnong’oneza mtu anayefuata na kuendelea hivyo. Yule mtu wa mwisho atarudia kile alichokisikia. Mchezo huu unaonyesha umuhimu wa kuwa msikilizaji mzuri. Unganisha mchezo huu na habari ya leo inayohusu mtu aliyetumia muda kusikiliza kwa umakini.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Martha na Mariamu walikuwa marafiki wazuri wa Yesu. Siku moja Martha alimwalika Yesu na wanafunzi Wake ili kula chakula kwa pamoja. Washirikishe Watoto katika kufikiri kuhusu baadhi ya maandalizi aliyoyafanya au husisha wazo la kwanza hapo juu. (Luka 10: 38)<br>• Martha alikuwa bado na mambo mengi ya kufanya! Alipokuwa akiendelea kuandaa chakula, umbu lake, Mariamu alikaa miguuni pa Yesu akisikiliza na kujifunza kutoka kwa yale ambayo Yesu alikuwa akisema. Elezea jinsi gani Martha alijihisi... labda watoto wanaweza kuhusianisha na hili! Tumia maneno yale yale aliyoyatumia Martha. (Luka 10: 39-40)<br>• Yesu alisema na Martha kwa upole, akamwambia hapaswi kusumbuka na kufadhaika. Eleza kwamba Martha alikuwa akifanya jambo jema katika kutaka kumpa Yesu chakula kizuri, Lakini halikuwa jambo la muhimu zaidi. Ni nani aliyechagua fungu lililo jema? Ndio, ni Mariamu! Yesu alisema kwamba Mariamu alichagua kufanya jambo ambalo ni bora na ambalo halitaondolewa kutoka kwake. (Luka 10: 41-42)<br>• Ni jambo gani jema Mariamu aliichagua? Mariamu alipata fursa ya kipekee kuweza kumsikiliza Yesu. Zungumza kuhusu jinsi gani tunapaswa kutumia muda kumsikiliza Yesu kwa kusoma na kujifunza kutoka kwenye Biblia. Na hapo tutamjua yeye zaidi na kujua kinachompendeza Bwana. Ukiwa na kundi la watoto wa umri mkubwa kidogo mnaweza kujadiliana jinsi wanavyoweza kulifanya jambo hili kuwa kipaumbele.<br><br>Kamilisha somo la Wakati na Biblia.<br><br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kujifunza kutoka kwa Yesu.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Fundisha na eleza, inapobidi, Mstari Muhimu Luka 10: 42. Thibitisha chaguo muhimu ambalo Mariamu alilifanya.</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Hawa dada waliishi wapi?<br>• Nani walikuwa wageni wao?<br>• Ni dada yupi alitumia muda na Yesu?<br>• Ni dada yupi alitaka kuhudumia Yesu?<br>• Ni dada yupi alifadhaika?<br>• Kwanini Martha alifadhaika?<br>• Martha alishitaki kwa nani?<br>• Tufuate mfano wa dada yupi?<br>• Tunawezaje kumsikiliza Yesu?<br>• Habari inapatikana katika kitabu gani cha Biblia?</td></tr>
</table>

**B3 Habari ya Pili**

**Uzima kupitia Yesu – Habari hii inahusu Yesu kumfufua mtu aliyekuwa amekufa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alikuwa na nguvu za kumfufua Lazaro.<br>• Yesu anaweza kutupa uzima wa milele ikiwa tunamtumaini Yeye.<br>.<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 11: 25***<br>**Neno la Biblia:** ***Yohana 11: 1-7, 17-44*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kwa daraja la 1, jadili jinsi ambavyo Mungu huwaweka watu katika familia. Zungumza kuhusu ndugu wa kiume na kike. Kuna mema gani kuhusu kuwa na ndugu wa kiume/kike? Waulize watoto kama wanakumbukumbu ya majina ya wale dada wawili katika habari ya wiki iliyopita na mtambulishe Lazaro.<br>• Kwa daraja la 2, zungumza kuhusu jinsi ambavyo mambo maishani mwetu hayaendi siku zote kama tulivyopanga – mara nyingine, mambo yasiyotarajiwa hutendeka ambayo yako nje ya uwezo wetu. Zungumza kuhusu jinsi Bwana Yesu alivyo na mamlaka ya kuongoza kila hali na hutenda mambo kwa manufaa yetu. Katika habari ya leo Mariamu na Martha walikuwa wanakabiliwa na tatizo gumu. |
| **FUNDISHA** | • Ndugu yao Mariamu na Martha aitwaye Lazaro alikuwa mgonjwa sana. Walimuhitaji Yesu aje kwa hiyo wakatuma ujumbe kwake. Walijua kuwa Bwana alikuwa na uwezo wa kumponya Lazaro. Lakini Yesu aliamua kutokuja! *Je walijisikiaje? Eleza kwamba ingawaje ilikuwa vigumu Mariamu na Martha kuelewa, Bwana Yesu alikuwa na mamlaka juu ya hilo na alijua lililo bora zaidi.* ***(Yohana 11: 1-6)***<br>• Punde Lazaro akafariki na akafungwa katika sanda na kuzikwa katika pango na jiwe kubwa likawekwa mlangoni. Tunaliita hili kaburi. *Kwa umakini mwingi jadili kwa kina jinsi gani Martha na Mariamu walivyojihisi sasa.* Siku nne baadaye, Martha alisikia kwamba Yesu anakuja, akaenda kumlaki. Yesu akamwambia kwamba Lazaro atafufuka na ataishi tena. *Tumia maneno aliyosema Yesu (Mstari 25) na eleza kwamba, ufufuo unamaanisha ile nguvu iwezayo kumrudisha mtu kutoka kwa wafu. Hakuna mtu mwingine yeyote aliye na nguvu hii!* ***(Yohana 11: 17-27)***<br>• Baadaye Yesu alikwenda kwenye kaburi la Lazaro akiwa pamoja na Mariamu na Martha. Yesu akalia machozi kwa sababu ya huzuni. Kisha Bwana akawaambia baadhi ya watu waliondoe jiwe halafu akaita kwa sauti kuu, “Lazaro, njoo huku nje!” Kwa mshangao wa kila mtu, Lazaro akatoka nje ya kaburi, akiwa bado amefungwa sanda. Sasa Yesu alidhihirisha kwamba anazo nguvu za kumrejeshea Lazaro uzima! Muujiza huu wa Yesu uliwasaidia kujua jinsi alivyokuwa na nguvu na alivyokuwa wa kipekee. ***(Yohana 11: 33-44)*** *Zungumza kuhusu yote aliyowafundisha kutokana na hili tukio – Muda muafaka Kwake, kushiriki huzuni yao, nguvu Yake, mamlaka Yake...Unaweza kuongezea kwa kusema kwamba kama Yesu angekuja kabla ya Lazaro kufa, muujiza huu usingehitajika!*<br>• Bwana Yesu anaweza kumkabili adui yetu mkubwa – mauti. Anayo nguvu ya kuishinda mauti, kama Alivyotudhihirishia Alipomrejeshea Lazaro uzima wake, na Yeye mwenyewe alipofufuka kutoka kwa wafu.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Uzima kupitia Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na kueleza, pale inapobidi, Mstari Muhimu. ***Yohana 11: 25***. Eleze kwamba Yesu anatuambia kweli ya muhimu sana kuhusu Yeye mwenyewe anapotumia jina Lake. Watoto wenye maarifa zaidi kuhusu Biblia wanaweza kuwa na kumbukumbu ya semi zingine za “Mimi ndimi”. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Ni nani alikuwa mgonjwa sana?<br>• Ilichukua muda gani kabla ya Yesu kuja?<br>• Ni dada yupi aliyekwenda kumlaki Yesu?<br>• Yesu alitumia jina gani kwa ajili Yake wakati alipokuwa akizungumza na Martha?<br>• Ni kwa jinsi gani Yesu alidhihirisha Alivyohisi akiwa kwenye kaburi la Lazaro?<br>• Alisema maneno gani?<br>• Ni jambo gani Yesu alithibitishia kila mtu siku hiyo?<br>• Tunawezaje kupata uzima wa milele? |

## B3 Habari ya Tatu

**Upendo kwa ajili ya Yesu – Habari hii inahusu: Mariamu alivyoonesha upendo wake kwa Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mariamu alionesha upendo wake kwa Yesu kwa kile alichokifanya<br>• Tunapaswa kumpenda Yesu katika kutambua upendo aliotuonesha sisi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 4: 19***<br>**Neno la Biblia:** ***Yohana 12: 1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu "zawadi za shukurani''. Kama itafaa, pata mifano ya zawadi za kawaida katika muktadha wa utamaduni wenu na uamue zawadi hizo zinawafaa akina nani.<br>Wakumbushe watoto habari ya wiki iliyopita na jinsi gani Mariamu, Martha na Lazaro walimshukuru Yesu. |
| **FUNDISHA** | • Mariamu, Martha na Lazaro waliamua kuandaa karamu (sherehe) kwa kumheshimu Yesu. Vuta taswira hiyo – nyumba hiyo ikiwa imejaa wageni, Lazaro akiwa buheri wa afya, Yesu akiwa kama mgeni wa heshima zaidi, Martha akitumikia... ***(Yohana 12: 1-2)***<br>• Wakati wa karamu hiyo, Mariamu alisogea karibu na Yesu, huku ameshikilia chupa ya marhamu ya thamani nyingi. Moja kwa moja, akaimimina miguuni kwa Yesu na akamfuta miguu kwa nywele zake. Fafanua ni kwa jinsi gani Mariamu alifanyika kivutio kwa wageni wengine waliogeuka kutazama kilichokuwa kikiendelea na kutambua kunukia kwa marhamu. Eleza kwamba Mariamu alifanya hili kwa sababu alimpenda Yesu sana – kwake Mariamu Yesu alistahili na alikuwa wa thamani kuliko kitu chochote kile. ***(Yohana 12: 3)***<br>• Yuda, aliyekuwa mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu, hakuweza kuelewa kwa nini Mariamu alimwaga marhamu. Kwake yeye ilionekana kana kwamba ni hasara! Nukuu maneno yale Yuda aliyosema na eleza kwamba Yuda alikuwa mlafi na mwizi.(Somo la Daraja la 2) ***(Yohana 12: 4-6)***<br>• Yuda na Mariamu walionesha tabia zilizotofautiana kwa Bwana Yesu. Yuda hakuweza kutambua ukuu wa Yesu na hakuwa na upendo kwa Yesu ndani ya moyo wake. Kwa Mariamu, upande wa pili, Yesu alikuwa wa thamani, na alimpenda Bwana sana. Yesu alipendezwa na kile Mariamu alichokifanya. ***(Yohana 12: 7-8)*** *Inafaa tufuate mfano wa nani?*<br>• *Tunapotafakari jinsi Bwana Yesu alivyotupenda na kuyatoa maisha yake ili kutuokoa, lazima awe wa thamani kwetu. Twaweza kumpenda kama mwitikio wa upendo wake kwetu, kama Mariamu alivyofanya. Zungumzia kuhusu njia ambazo twaweza kuonesha upendo wetu kwa Yesu. kwa mfano kumtumaini Yesu, kuwa na muda na Yesu kwa kuomba na kusoma Neno Lake, Kumtii, kuwapenda wengine na kuwaambia kuhusu Yesu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Upendo kwa ajili ya Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na eleza, pale inapobidi, Mstari Muhimu. ***1 Yohana 4: 19***. Hakikisha watoto wameelewa nani ametajwa kama "Bwana". Eleza kwamba upendo wetu ni matokeo ya Upendo Wake kwetu. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Karamu ilifanyikia wapi?<br>• Ni nani alikuwa mtu wa muhimu mahali hapo?<br>• Mariamu alifanya nini?<br>• Kwanini Mariamu alifanya hili?<br>• Yuda alisema nini kuhusu Mariamu kumpaka Yesu marhamu?<br>• Kwa nini inatupasa kumpenda Bwana Yesu? |

**B3 Habari ya Nne**

**Kumtazama Yesu – Habari hii inahusu Yesu Kukaribishwa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu ni wa pekee – Yeye ni Mfalme wa Wafalme.<br>• Tunahitaji kumkaribisha Bwana Yesu maishani mwetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 1: 12***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 19: 28-44*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu jinsi wageni muhimu wanavyokaribishwa – kwa mfano, mgeni wa kifalme, rais, mwanamichezo bingwa, mgeni anayekuja shuleni. Tumia baadhi ya picha kama zinapatikana. Jitahidi kuleta picha ya wazo la jinsi ambavyo ingelikuwa mtu kuwa sehemu ya umati wa watu.<br><br>Eleza ya kwamba kwa tukio hili Yesu alikuwa mgeni wa pekee. Alikuwa akiingia mji wa Yerusalemu kwa mara ya mwisho kwa sababu kitambo kidogo utakuwa ni muda Wake wa kutimiza mpango wa Mungu wa kufa kwa ajili ya dhambi zetu.<br>Mungu alitaka watu wajue jinsi Yesu alivyo wa pekee. Biblia inamuita “Mfalme wa wafalme na Bwana wa Mabwana. Mungu alikuwa amepanga mpango mahususi jinsi gani Yesu ataingia Yerusalemu siku hii ya muhimu ili watu waweze kumtambua. |
| **FUNDISHA** | • Yesu na wanafunzi wake walipokaribia Yerusalemu, Alituma wanafunzi wawili waende katika kijiji ambapo watamkuta mwanapunda amefungwa. Maagizo ya Yesu yalikuwa wamfungue na kumleta Kwake na kama mtu akiwauliza kwanini wanamfungua, jibu lao lingelikuwa, “Bwana ana haja naye.” ***(Luka 19: 28-31)***<br>• *Tafakari kwa namna gani wanafunzi walimpata huyo mwanapunda na kumleta kwa Yesu. Ni kwa namna gani mwanapunda angefanya pale mtu anapokaa juu yake kwa mara ya kwanza? Wanafunzi wakatandika nguo zao juu ya mwanapunda zitumiwe kama tandiko na yule mwanapunda alikubali Yesu akae mgongoni mwake.* Hii haikuwa kawaida, lakini Yesu alikuwa na uwezo juu ya viumbe vyote! ***(Luka 19: 32-35)***<br>• Ikawa Yesu alipokuwa amempanda mwanapunda, umati wa watu walitandaza nguo zao njiani, ikawa kama wametengeneza zulia. Hapo sasa yale makusanyiko wakamjua Yesu – Mfalme wa pekee aliyetumwa na Mungu. *Eleza kwamba mfalme hupanda juu ya farasi anapokwenda vitani, bali kwa kupanda juu ya punda Yesu alionesha kwamba Yeye ameleta amani.* Watu walijawa na furaha na kumsifu Mungu kwa sauti kuu wakisema, “Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana.” ***(Luka 19: 36-38)***<br>• *Taja kwamba palikuwepo na wengine ambao hawakumpenda Yesu na walikasirishwa na kitendo cha Yesu kukaribishwa.* ***(Luka 19: 39-40)*** Yesu alijua kwamba watu hawa kitambo kidogo wangelifanikiwa kumuua.<br>• *Wape changamoto watoto kwamba sisi tunao uchaguzi wa muhimu wa kufanya kuhusu Bwana Yesu. Tunaweza kuchagua kumkaribisha ndani ya maisha yetu au kusema “La” Kwake na kutompa nafasi. Mungu anataka tumualike Mwanawe ndani ya maisha yetu.Tunapofanya hivyo tunafanyika sehemu ya familia ya Mungu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kumtazama Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na eleza, pale inapobidi, Mstari Muhimu. ***Yohana 1: 12***. Eleza kwamba maneno haya pokea, kubali au amini yote yana maana moja ya kukaribisha. Hakikisha kwamba viwakilishi (Kwake, Yeye) vinaeleweka. |
| **KUMBUKA** | Jibu kweli au si kweli katika sentensi za jaribio hili.<br>• Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakiingia Yerusalemu.<br>• Yesu alituma wanafunzi Wake watatu waende kijijini.<br>• Walipanda punda.<br>• Punda hakusumbua Yesu alipokaa juu yake.<br>• Watu waliweka zulia njiani.<br>• Kila mtu alimkaribisha Yesu.<br>• Yesu ni Mfalme wa Wafalme na anapaswa kukaribishwa.<br>• Tunapomkaribisha Yesu ndani ya maisha yetu tunafanyika sehemu ya familia ya Mungu. |

## B4 Habari ya Kwanza
**Kufa kwa Yesu - Habari hii inahusu Yesu kutufia.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alitendewa vibaya na hakustahili kufa.<br>• Bwana Yesu alikufa ili kutuokoa na dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 23: 33***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 23:1-26, 32-43*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Uwe na kadi kadhaa zilizoandikwa maneno yafuatayo: **kukatishwa tamaa na rafiki, kushitakiwa kwa uongo, kudhihakiwa, mtu fulani kukutenda vibaya.** Toa mifano ya mambo haya katika maisha ya kila siku, au katika kikundi kidogo, watoto wanaweza kushirikisha uzoefu wao na jinsi walivyojisikia kutendewa hivi. Tungetaka kuzuia yasitokee!<br>Eleza kwamba Bwana Yesu alijua maumivu ya kutendewa vibaya. Watu walimfanyia mambo haya yote na mengine mabaya zaidi. Leo tutajua ni kwanini aliteswa hivi. |
| **FUNDISHA** | (Kama unafundisha shuleni itafaa kuwa na kalenda ya matukio ya mlalo au usawa (horizontal kwa Lugha ya kiingereza) ili kuonesha mpangilio wa matukio kadiri unavyofundisha. Maelezo mafupi kwenye kadi yenye michoro rahisi yaliyochorwa kwa kutumia vimistari (line drawings kwa Lugha ya Kiingereza) kama vile **chakula maalum cha jioni, kuomba katika bustani, kukamatwa na maadui, kuhojiwa na Pilato, umati wa watu wenye hasira, kuchukuliwa ili kusulibiwa, misalaba mitatu, mwizi aliyesamehewa** yatawawezesha watoto kukumbuka muendelezo wa matukio na maelezo.)<br>• *Uliza maswali machache ili kuwakumbusha watoto kuhusu kuingia Yerusalemu.* Siku chache baadaye Yesu alikula chakula maalum cha jioni na wanafunzi wake, mwishoni kabla ya kufa kwake. Kisha akaenda kwenye bustani kuomba. *Onesha tukio lilivyokuwa - giza, ukimya, halafu nyayo zinasikika na nafasi ya Yuda katika kukamatwa kwa Yesu. Onesha huzuni ambayo kwa vyovyote vile Yesu alikuwa nayo.* ***Luka 22: 7-20, na 22: 39-53***<br>• Siku iliyofuata, Yesu alipelekwa kwa Pilato aliyekuwa Gavana. ***(Luka 23: 1-4, 20-25)*** *Eleza mamlaka yake ya kufanya maamuzi na uzingatie ukweli kwamba hakuweza kupata makosa yoyote katika maisha ya Yesu. Bwana Yesu alikuwa mkamilifu na hakuwa na dhambi.* Mwishowe, Pilato alifanya kile ambacho umati wa watu wenye hasira ulitaka hivyo akamhukumu Yesu kifo. Kwetu inaonekana kama haki haikutendeka lakini ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu ili kutuokoa!<br>• Yesu alichukuliwa nje ya Yerusalemu. Mtu aliyeitwa Simoni alilazimishwa kubeba msalaba mkubwa wa mbao. ***(Luka 23: 26)*** Walipofika kwenye kilima, askari walimsulibisha Yesu msalabani. Wezi wawili pia waliuawa wakati huo huo, mmoja upande wa kushoto na mwingine upande wa kuume wa Yesu. Yesu alipokuwa akining'inia msalabani askari walimdhihaki na hata mmoja wa wezi alikuwa mkorofi. Mwizi mwingine alijua kwamba Yesu hakuwa kama wao. Alielewa kuwa alikuwa akifa kwa sababu alikuwa amefanya vibaya lakini Yesu hakufanya chochote kibaya. Alitambua Yesu alikuwa nani na akamwomba Yesu amkumbuke. Yesu aliahidi kwamba siku hiyo hiyo, atakuwa Mbinguni pamoja Naye. ***(Luka 23: 32-43)***<br><br>*Eleza kwamba kama alivyofanya mwizi, tunahitaji kuelewa kwamba Yesu hakustahili kufa. Badala yake aliteswa na kufa ili aweze kutuonesha upendo mkuu wa Mungu na kuchukua adhabu ya dhambi zetu. Ikiwa tutamwomba atusamehe, sisi pia tunaweza kuwa na hakika kwamba siku moja tutakuwa Mbinguni.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Upendo wa Yesu / Kufa kwa Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na ueleze, inapofaa, Mstari Muhimu. ***Luka 23: 33***, au sehemu yake, kulingana na uwezo wa watoto. Elezea jina la kilima ambapo Yesu alikufa. Mstari mbadala utakuwa ***1 Petro 3:18.*** |
| **KUMBUKA** | Changanya zile kadi zenye maelezo mafupi kisha uwaambia watoto wazipange kwa usahihi. Ikiwa unafanya kazi na kikundi kidogo cha watoto, unaweza kuwa na nakala kwa timu tofauti ambapo timu itakayopanga kwa haraka zaidi ndiyo itakuwa mshindi. |

## B4 Habari ya Pili
**Yesu afa na kuzikwa - Habari hii inahusu kifo na kuzikwa kwa Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kifo cha Yesu kilikuwa tofauti na kingine chochote kwa sababu alichukua adhabu ya dhambi zetu.<br>• Tunatakiwa kumshukuru kwa upendo wake mkuu kwetu.<br><br>**Mistari Muhimu:** ***1 Wakorintho 15: 3 & 4***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 23: 44-56*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu mchana na usiku, jinsi zinavyofuatana. Tunatarajia usiku uje katika wakati fulani! Hivyo ndivyo Mungu alivyoumba iwe. Lakini siku ambayo Yesu alikufa ilikuwa tofauti. Ghafla bila tahadhari yoyote, saa 6 mchana, jua liliacha kuangaza na ilikuwa giza kama usiku. Hali hii ilidumu kwa masaa matatu.<br>***(Luka 23: 44, 45)*** Kwa nini Mungu aliruhusu jambo hilo litendeke? |
| **FUNDISHA** | • Biblia inatuambia kwamba, katika masaa haya matatu Bwana Yesu aliadhibiwa na Mungu kwa ajili ya dhambi zetu. *Wakumbushe watoto namna ambavyo Yesu aliteseka katika habari ya wiki iliyopita. Elezea kwamba tunaweza kuelewa kidogo kuhusu yale mateso ambayo alikuwa ameteseka lakini hatuwezi kuelewa adhabu ya dhambi zetu. Yesu alichukua adhabu hii kwa hiari kwa sababu alitupenda na alitaka kutimiza mpango wa Baba yake ili tuokolewe.*<br>• Mwishowe, Yesu aliomba na kumkabidhi Mungu roho yake. ***(Luka 23: 46)*** Hii ilikuwa njia ya Yesu kusema kwamba alikuwa amemaliza kazi ambayo Baba yake alimtuma kuifanya. *Sema kuhusu utoshelevu unaopatikana katika kukamilisha kazi rahisi, ukijua kuwa hakuna kitu kingine kinachohitajika kufanywa – kama vile, kutengeneza mfano. Yesu alikuwa amefanya <u>kila kitu</u> kinachohitajika ili dhambi zetu zisamehewe. Wape changamoto watoto juu ya hitaji lao la kupokea kile ambacho Yesu amefanya kwa niaba yao.*<br>• Kisha Yesu akafa. Chunguza jinsi marafiki zake walivyojisikia. Rafiki mwema aliyeitwa Yusufu alikwenda kwa Pilato na kuomba mwili wa Yesu. Kwa uangalifu aliushusha mwili kutoka msalabani, akaufunga kwa kitambaa cha kitani na kuuweka kwenye kaburi jipya. *Eleza kwamba kaburi lilikuwa kama pango dogo.* Kisha akavingirisha jiwe kubwa mlangoni. ***(Luka 23: 50-53)***<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufa kwa Yesu / Yesu afa na kuzikwa. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na ueleze, inapofaa, Mistari Muhimu. ***1 Wakorintho 15: 3 & 4***. Watoto wadogo wanaweza kusema maneno matano ya kwanza. Hakikisha watoto wanajua Maandiko yana maana gani na ueleze kwamba yote yaliyompata Bwana Yesu yalikuwa yameandikwa katika Agano la Kale miaka mingi iliyopita. |
| **KUMBUKA** | Jibu kweli au si kweli katika sentensi za jaribio hili.<br>• Giza lilianza katikati ya mchana.<br>• Lilichukua masaa manne.<br>• Wakati wa giza, Yesu alichukua adhabu ya dhambi zetu.<br>• Yesu alizungumza na Baba Yake kabla hajafa.<br>• Marafiki wa Yesu walielewa kila kitu kilichompata.<br>• Yusufu aliwaomba askari wampatie mwili wa Yesu.<br>• Aliufunga mwili kwenye kitambaa cha kitani.<br>• Aliuweka mwili ndani ya kaburi la zamani. |

## B4 Habari ya Tatu
**Yesu afufuka – Habari hii inahusu Mariamu kugundua kuwa Yesu yu hai!**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimfufua Yesu siku ya tatu baada ya kifo chake.<br>• Kama vile Mariamu alivyogundua kuwa Bwana amefufuka, sisi pia tunaweza.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 10: 9***<br>**Neno la Biblia:** ***Yohana 20: 1-18*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Katika habari yetu ya mwisho tulijifunza juu ya Yesu kufa msalabani. Eleza kwamba kwetu hii ni habari njema! Kupitia kifo cha Yesu msalabani, Mungu aliweza kutupatia njia ili dhambi zetu zisamehewe. Mpango wa ajabu wa Mungu ulikuwa umekamilika!<br>Marafiki wa Yesu, walifadhaika na kuhuzunika. Hawakuweza kuelewa mambo hayo kama sisi tunavyoweza kuyaelewa sasa kwa msaada wa Biblia. Lakini hawakulazimika kukaa na huzuni kwa muda mrefu! Habari hii ina mwisho bora wa aina yake! |
| **FUNDISHA** | • *Wakumbushe watoto kuhusu kuzikwa kwa Yesu na kaburi lenye jiwe kubwa.* Siku hiyo ilikuwa asubuhi ya Jumapili, siku ya tatu baada ya Yesu kufa. Mariamu, rafiki mzuri wa Yesu, alienda kutembelea kaburi. *Eleza mshangao wake kugundua kuwa jiwe lilikuwa limevingirishwa pembeni na kaburi lilikuwa tupu.* Mariamu alikimbia kumtafuta Petro na Yohana ili kuwaambia kile alichogundua. Tumia maneno aliyosema. ***(Yohana 20: 1-2)*** *Walijisikiaje kuhusu habari hii?*<br>• Petro na Yohana walifurahishwa na habari hii na wakakimbia haraka walivyoweza. Yohana alifika kwanza na kutazama ndani ya kaburi lakini Petro alipofika huko, aliingia ndani! Vyote vilivyokuwako ndani vilikuwa ni vipande vya kitani ambavyo vilikuwa vimefungwa kwenye mwili wa Yesu. Kisha Yohana akaingia ndani pia. Mara Yohana akajua kile kilichokuwa kimetokea. Akajua kwamba Yesu alikuwa amefufuka! ***(Yohana 20: 3-9)***<br>• Lakini bado Mariamu alikuwa akishangaa. Alikaa kwenye bustani baada ya Petro na Yohana kurudi nyumbani. Alisimama akilia kisha akatazama tena kaburini. Wakati huu, Mariamu alipata mshangao mwingine. *Waelezee malaika wawili na ushirikishe mazungumzo yake na malaika hao.* ***(Yohana 20: 10-13)***<br>• Mariamu akiwa peke yake, akageuka. Kulikuwa na mtu amesimama kwenye bustani ambaye hakumjua. *Simulia mazungumzo.* Wakati huo mgeni huyo alitaja jina lake. "Mariamu!" Mara akaitambua sauti hiyo. Alikuwa ni Mwalimu wake, Bwana Yesu! *Je! Mariamu alijisikiaje sasa?* Mariamu alikuwa amejawa na furaha! Alikuwa yeye mwenyewe amemwona Bwana. Alikuwa amefufuka kweli kweli! Kwa mara ya pili Mariamu alienda kuwatafuta wanafunzi. *Je, aliwaambia nini wakati huu?* ***(Yohana 20: 14-18)***<br>• *Mungu alimfufua Bwana Yesu kutoka kwa wafu. Leo yuko hai. Biblia inasema Yeye yu hai milele na milele! Anataka kujaza furaha katika maisha yetu kama vile Mariamu alivyokuwa wakati alipokutana naye kaburini. Wape changamoto watoto juu ya kuwa na Bwana Yesu kama rafiki na yote ambayo anataka kutupatia - msamaha wake, nguvu na furaha.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yesu afufuka kutoka kwa wafu / Yesu afufuka. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapofaa, Mstari Muhimu. ***Warumi 10: 9***. Eleza kwamba "kukiri" inamaanisha kuwafanya wengine wajue kwamba tunaamini Yesu ni Bwana. Mstari huu unatufundisha kwamba tunatakiwa kuamini kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu ili kutuokoa kutoka kwenye adhabu ya dhambi zetu. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Ni nani aliyeenda kaburini kwanza?<br>• Je! Mariamu aligundua nini kuhusu jiwe?<br>• Alikwenda kumwambia nani?<br>• Ni nani aliingia kaburini kwanza?<br>• Je! Yohana alifanya nini alipogundua hakuna mwili ndani ya kaburi?<br>• Je! Mariamu aliona nini kaburini wakati akiwa peke yake?<br>• Malaika walimuuliza nini Mariamu?<br>• Ni nani alikuwa bustanini na Mariamu?<br>• Alijuaje kuwa ni Yesu?<br>• Ni nani alimfufua Yesu? |

## B4 Habari ya Nne
**Kwenda na kurudi kwa Yesu - Habari hii inahusu kurudi kwa Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Bwana Yesu aliendа Mbinguni na bado yuko huko.<br>• Tunatakiwa kuwa tayari kwa ajili ya kurudi kwake.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 1: 11***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 24: 50-53, Matendo 1: 4-12*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu kuagana kwa kuwasilisha hali – kwa mfano, ndugu amekaa na wewe na lazima arudi nyumbani kwake au mmojawapo katika darasa lako shuleni anaondoka na kwenda mbali. **<u>Au</u>** shirikisha tukio la kweli kutokana na uzoefu wako mwenyewe. Labda mtu huyo anaahidi kurudi wakati fulani au kuendelea kuwasiliana na wewe. Ahadi inafanya kuagana kuwe rahisi! |
| **FUNDISHA** | • Wanafunzi wa Yesu walipata muda mzuri na wakipekee kuwa pamoja Naye baada ya kufufuka. Sasa walielewa zaidi kwa nini alikuwa amekufa. Karibu wiki sita baadaye, Aliwachukua wale wanafunzi kumi na mmoja kwenda kwenye kilima kiitwacho Mlima wa Mizeituni. Aliwaelezea kuwa wakati umefika wa Yeye kurudi Mbinguni. Wasingebaki peke yao kwa sababu punde msaidizi maalum anayeitwa Roho Mtakatifu alitarajiwa kuja kwao. Ghafla, wakati Yesu alipokuwa anazungumza nao, aliinuliwa juu kutoka chini. *Fikiria jinsi walivyotazama angani kisha wakati huo Yesu akawa amefichwa machoni pao na wingu. Unaweza kutaja ukweli kwamba Yesu alipaa kwenda Mbinguni. (Daraja la 2) Tafakari jinsi walivyohisi – walichanganyikiwa? walishangaa? walihuzunika?* ***(Matendo 1: 8-9)***<br>• Wakati huo malaika wawili walitokea na kuwauliza wanafunzi kwa nini walikuwa wamesimama wakitazama angani. Ndipo malaika wakawaambia kwamba Yesu atarudi tena kwa njia ile ile aliyoondoka. ***(Matendo 1: 10-11)***<br>Wanafunzi walijua kwamba hawapaswi kukaa kwenye kilima lakini badala yake wanapaswa kwenda Yerusalemu kupokea Msaidizi ambaye Yesu alikuwa ameahidi. Hawakuwa na huzuni lakini walikuwa wamejaa furaha! ***(Luka 24:52)*** Husianisha hili na mjadala wako wa utangulizi kuhusu kuondoka kwa watu. Eleza kwamba waliamini kwamba Yesu atatimiza neno Lake kwao.<br><br>Bwana Yesu bado yuko Mbinguni mpaka leo lakini wale wampendao wanangojea kurudi kwake. Hatujui itakuwa ni lini lakini tunajua kwamba itatokea - Atatimiza ahadi Yake. *Wape changamoto watoto juu ya kuwa tayari kwa ajili ya kurudi kwake na uhakikishe kwamba wanajua jinsi ya kuwa tayari - kwa kumwamini Bwana Yesu awasamehe dhambi zao.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kwenda na kurudi kwa Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapofaa, Mstari Muhimu. ***Matendo 1: 11***. Huu ni mstari mrefu - chagua sehemu ya mstari ambao watoto katika kikundi chako wanaweza kuushika n.k. kuanzia na "Yesu huyu huyu ....." (Daraja la 2) au maneno ya malaika kama yalivyotolewa katika Daraja la 1. Wakumbushe watoto muktadha wa mstari - ni nani aliyesema, ulisemwa kwa nani, ulisemwa lini / wapi. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Wanafunzi wangapi walikuwa na Yesu kwenye Mlima wa Mizeituni?<br>• Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba anaondoka akiwa wapi?<br>• Aliwaahidi kupokea nini?<br>• Ni nini kilimficha wasimuone?<br>• Malaika waliwapa ujumbe gani?<br>• Wanafunzi walikwenda wapi baada ya hapo?<br>• Yesu atarudi lini?<br>• Anakuja kwa ajili ya nani? |

## B5 Habari ya Kwanza

**Msamaria Mwema – Habari hii inahusu kumpenda jirani yako.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Jirani wa kweli ni mtu yeyote anayeonesha huruma kwa mtu mwenye hitaji.<br>• Yesu anatutaka tuwahurumie wengine.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 10: 27***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 10: 25-37*** |
| **TOA UTANGULIZI** | **<u>Daraja la 1:</u>** Waambie watoto wazungumze kuhusu majirani zao nyumbani. Majirani wanasaidianaje? Kiongozi anaweza kuchora picha rahisi kuelezea mawazo ya watoto, au mtoto mwenye wazo fulani anaweza kuonesha kwa vitendo na wengine wakisie ana maana gani.<br>**<u>Daraja la 2:</u>** Zungumza jinsi hadithi zinavyovutia na zinavyoweza kuburudisha. Waulize watoto kuhusu hadithi wanazozipenda zaidi. Eleza kwamba Yesu alisimulia Habari nyingi ambazo ziliwasaidia watu kuelewa kuhusu Mungu na jinsi wanavyopaswa kuishi. Habari hizi zinaitwa **<u>mifano</u>**. Siku moja mtu alikuwa akizungumza na Yesu. Alijua sheria ya Mungu ilivyosema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." ***(Luka 10:25-28)*** Waulize watoto kama wanajua sehemu ya kwanza ina maana gani. Huyu mtu hakujua vizuri jirani yake ni nani hivyo Yesu akamwambia mfano ili kumsaidia kuelewa. |
| **FUNDISHA** | • Mtu mmoja alisafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. *Eleza kwamba hii ilikuwa ni barabara ya hatari, yenye mteremko mkali na upepo, na mara kwa mara kulikuwa na wanyang'anyi wanaovizia. Igiza unapokuwa ukiwaambia jinsi ghafla huyu mtu alivyokamatwa, akapigwa, akanyang'anywa na kuachwa karibu ya kufa kando ya barabara. Muda ukiruhusu mnaweza kujadili nini kingefuata kama jambo hili lingetokea kipindi hiki.* ***(Luka 10:29-30)***<br>• Punde, mtu alipita, akaona kilichotokea lakini hakufanya chochote kumsaidia mtu huyu aliyejeruhiwa! Muda mfupi baadaye, mtu mwingine akashuka katika njia ile. Wasafiri wote wawili walipita kando ya barabara bila kumsaidia. La kusikitisha zaidi watu hawa wote walikuwa wanatumika katika Hekalu la Mungu. ***(Luka 10:31-32)***<br>• Mtu wa tatu ambaye alipita hapo alitoka nchi nyingine. Kwa wale wa daraja la 2 unaweza kuwaeleza kwamba alikuwa Msamaria na kwa kawaida Wasamaria na Wayahudi (aliyejeruhiwa akiwa mmoja wao) hawakushirikiana. Usingetegemea Myahudi na Msamaria kusaidiana! Hata hivyo, Msamaria yeye alisimama. Alitoa huduma ya kwanza, akampandisha yule mtu juu ya punda wake na kumpeleka nyumba ya wageni ambapo aliendelea kumtunza usiku ule. *Ashiria namna alivyotoa muda wake na pesa zake na kuhakikisha kuwa huyu mtu anapona. Inafaa kuwa na sanduku la vifaa vya huduma ya kwanza unapowafundisha watoto wadogo.* ***(Luka 10:33-35)***<br>• Yesu alipomaliza kusimulia hii habari aliuliza yupi kati ya wale wasafiri watatu alikuwa jirani wa huyu mtu. *Waulize watoto wangejibuje na thibitisha kwamba yule mtu alitoa jibu sahihi pia. Kisha Yesu akamwambia aende na kufanya hivyohivyo. Wasaidie watoto wa daraja la 1 kuelewa kwamba jirani ni mtu yeyote mwenye huruma ... sio lazima aishi nyumba ya jirani. Waulize watafakari kuhusu njia ambazo wanaweza kuonyesha huruma kwa wengine darasani na uwanjani.*<br>• *Watoto wa daraja la 2 wanaweza kutafakari hali ambayo inaweza kuwa vigumu kuonesha huruma kwa watu na ukweli kwamba Yesu anatufundisha kumhurumia kila mtu, sio tu wale wanaotuhurumia. Wanaweza pia kufikiri njia zozote ambazo Bwana Yesu anafanana na Msamaria Mwema. (Mwokozi, Msaidizi na Rafiki)*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Msamaria mwema. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. ***Luka 10: 27***. Watoto wa Daraja la 1 wanaweza kujifunza sehemu ya mwisho ya mstari huu. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari<br>• Habari alizosema Yesu zilipewa jina gani?<br>• Mtu aliyekuwa safarini alikuwa akienda wapi?<br>• Jambo gani lilimpata?<br>• Ni wanaume wangapi walipita karibu naye bila kumsaidia?<br>• Ni mtu yupi alisimama kusaidia?<br>• Alifanya nini?<br>• Alimpa sarafu ngapi mwenye nyumba ya wageni?<br>• Yesu alimwambia nini yule mtu mwishoni mwa habari ile? |

**<u>B5 Habari ya Pili</u>**

**Kondoo Aliyepotea – Habari hii inahusu jinsi Bwana Yesu anavyotujali.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Sisi ni kama kondoo waliopotea kwa sababu tunafuata njia zetu badala ya njia ya Mungu.<br>• Yesu ni Mchungaji Mwema ambaye anataka kutupata.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 10: 11***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 15: 1-7*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili - Je! Umewahi kupotea? Ilitokeaje? Ulijisikiaje? Nani alikupata? Ulijisikiaje ulipopatikana?<br>Waambie watoto kwamba habari ya leo inahusu mchungaji aliyepoteza kondoo.<br>Waulize ni kitu gani wanafikiri mchungaji angelazimika kufanya ili kuchunga kondoo. (kulisha, kulinda, kutunza nk.)<br>Waeleze watoto kwamba kondoo mara nyingi hutangatanga kutoka mahali wanapopaswa kuwa na kujikuta wakipotea. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja watoza ushuru na wenye dhambi walikuja kumsikiliza Yesu. Watu wengine wakaanza kunung'unika na kulalamika kwa sababu Yesu alikuwa akiwakaribisha wenye dhambi. Hakupenda manung'uniko yao hivyo akaanza kuwaambia watu habari. ***(Luka 15: 1-3)*** *Eleza watoto kwamba Yesu anataka kila mtu aje kwake. Haijalishi wao ni nani au wamekosea nini.*<br>• Alisimulia habari kuhusu mchungaji ambaye alikuwa na kondoo 100. Siku moja mmoja wao alipotea. Mchungaji aliwaacha kondoo wengine wote na kwenda kumtafuta yule aliyepotea. *Ashiria baadhi ya sehemu ambazo inawezekana alienda kumtafuta. Elezea zaidi kwa kutia mkazo kuhusu uvumilivu wake aliouonesha. Hakuwa na furaha mpaka alipompata.* ***(Luka 15: 4)***<br>*Waambie watoto kwamba Biblia inasema sisi ni kama kondoo waliopotea. Bwana Yesu ndiye Mchungaji Mwema na anataka kutupata na kutulea. Waulize watoto waainishe njia ambazo Yesu anaonesha kutujali. Unaweza kuziandika na kuwahimiza watoto kushukuru kwa malezi Yake. (Hakikisha unaonesha bayana kwamba njia kuu ambayo Yesu aliitumia kutujali ni kwa kutoa uhai wake kwa ajili yetu.)*<br>• Mwishowe alipompata kondoo alifurahi sana. Akamuinua kondoo juu, akamweka juu ya mabega yake na kumchukua kwenda nyumbani. Alipofika nyumbani akawaita marafiki na majirani zake wote ili kusherehekea kwa sababu alikuwa amepata kondoo wake aliyekuwa amepotea. ***(Luka 15: 5-6)***<br>• *Waambie watoto kwamba kama vile mtu huyo alivyofurahi sana alipompata kondoo wake aliyepotea, kuna furaha ya kweli Mbinguni wakati mmoja wetu anapotubu na kuomba msamaha wa mambo mabaya ambayo amefanya na kumtumaini Yesu. Kwa watoto wadogo, unaweza kusimulia habari kwa ushiriki wao: kwa kuhesabu, kama wanajua kuhesabu hadi 99, na vitendo vya kuchunga, kupanda juu, kutafuta, kupata, na kusherehekea.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kondoo aliyepotea. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. ***Yohana 10: 11.*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Kwa nini watu wengine hawakufurahi?<br>• Mchungaji alikuwa na kondoo wangapi?<br>• Ni wangapi walipotea?<br>• Mchungaji alifanya nini alipogundua kuna kondoo amepotea?<br>• Alimbebaje kondoo hadi nyumbani?<br>• Alifanya nini alipofika nyumbani?<br>• Ni nani anafananishwa na kondoo?<br>• Ni nani anafananishwa na mchungaji? |

**B5 Habari ya Tatu**

**Mwana Mpotevu – Habari hii inahusu kujuta kwa kufanya vibaya.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu anatutaka tuseme tunasikitika kwa mambo mabaya ambayo tumefanya.<br>• Mungu atatusamehe kila wakati tunapomwambia tunajutia mabaya tuliyotenda.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 15: 24***<br>**Neno la Biblia:** ***Luka 15: 11-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie watoto habari fupi rahisi kuelezea wazo la msamaha. *Mfano, Siku moja Neema na Baraka walikuwa wakicheza pamoja. Neema alianza kucheza na mpira ambao Baraka aliutaka. Baraka akakasirika. Akampokonya Neema mpira na kumwangusha. Neema akaanza kulia.* Jadili - Kwanini Neema alilia? Unafikiri Baraka alipaswa kufanya nini? Je! Unadhani Neema alipaswa kumsamehe? Waambie watoto kwamba habari ya leo kutoka kwenye Biblia inahusu msamaha. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alisimulia mfano mwingine. Kulikuwa na mtu ambaye alikuwa na wana wawili. Mwana mdogo alimwomba baba yake pesa ambazo siku moja zingekuwa zake. Baba akampa pesa zake. *Jadili jinsi mtoto na baba walivyohisi.* ***(Luka 15: 11-12)***<br>• Muda si mrefu baada ya hapo, mwana huyo aliweka vitu vyake vyote kwenye mabegi yake na kwenda safari ndefu. Wakati akiwa mbali alitumia pesa zake zote kwa njia mbaya. Kisha kukawa na janga la njaa katika nchi hiyo. *Eleza janga la njaa ni nini. Elezea alitambuaje pesa zake zimekwisha, na tatizo lililompata. Jadili – Unafikiri huyu mwana mdogo alijisikiaje alipotambua hajabakiwa na kitu? Unafikiri alipaswa kufanya nini?*<br>• Huyu kijana hakuwa na mtu yeyote wa kumuomba msaada. Ilibidi ajipatie kazi ya kulisha nguruwe. Wakati mwingine alikuwa na njaa kiasi kwamba alitamani kula chakula cha wanyama. ***(Luka 15: 13-16)***<br>• Siku moja alianza kufikiria kuhusu nyumbani kwao. *Wasaidie watoto kupata picha ya namna mwana mdogo alivyoonekana akiwa anarudi nyumbani kwao. Linganisha na safari yake wakati akitoka nyumbani kwao.* Alitambua kuwa hata watumishi pale nyumbani kwao walikuwa na chakula cha kuwatosha. Aliamua kwenda nyumbani kwa baba yake, kumwambia anajuta na akamwomba kama angeweza kuwa mmoja wa watumishi wake. Baba yake alimwona akija akiwa bado mbali. Baba yake akamkimbilia na kumbusu. Mwana huyo alianza kusema anajuta, lakini baba yake akamnyamazisha. Akatoa wito kwa watumishi kuleta vazi bora, pete na viatu kwa ajili yake na akaandaa tafrija kubwa ya kusherehekea mtoto wake kurudi nyumbani. ***(Luka 15: 20-24)*** *Waulize watoto waoneshe jinsi baba alivyomfanyia mwanae. (mfano, huruma, ukarimu, msamaha, furaha isiyo kifani)*<br>• *Jadili - Unafikiri mwana alijisikiaje mara tu aliporudi nyumbani? Waeleze watoto kwamba sisi ni kama huyo mwana kwa sababu tumetenda mambo mabaya. Mungu ni kama Baba. Yeye anataka tumwendee na kumwambia tunayajutia mabaya tuliyotenda. Jadili –Umewahi kujaribu kusema samahani kwa mtu lakini hakukusikiliza au hakukusamehe? Waambie watoto kuwa Mungu hutusikiliza na kutusamehe SIKUZOTE tunapomwambia kwamba tunajutia mabaya tuliyotenda.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mwana mpotevu/ Mwana mpumbavu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Luka 15: 24***. Eleza kwamba baba hakujua kilichompata mtoto wake - ilikuwa kama amekufa. Lakini sasa kwa kuwa amerudi, alikuwa mzima na hai kwelikweli! |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Yule mtu alikuwa na wana wangapi?<br>• Yule mwana mdogo alimwomba nini baba yake?<br>• Mwana alifanyia nini pesa zake?<br>• Alipata kazi gani?<br>• Je! Aliamua kufanya nini wakati huo?<br>• Je! Baba yake alifanya nini alipomwona mwanawe anarudi nyumbani?<br>• Je! Baba alimpa nini mwanae?<br>• Baba katika habari ni kama nani? |

**B5 Habari ya Nne**

**Mpanzi – Habari hii inahusu kile tunachofanya kwa kutumia Neno la Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Biblia ni Neno la Mungu.<br>• Mungu anataka tuwe kama udongo mzuri na tuamini yale anayotuambia katika Biblia.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 4: 20***<br>**Neno la Biblia:** ***Marko 4: 1-20*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili - Je! Umewahi kujaribu kukuza mmea? Ulikuza mmea gani? Je! Mmea huo ulihitaji nini ili kukua? Je! mmea ulikua vizuri au ulikufa? Au ukiwa na kikundi kidogo unaweza kuonesha mbegu tofauti.<br>Waeleze watoto kwamba habari ya leo inahusu mkulima ambaye alijaribu kupanda mazao kadhaa. |
| **FUNDISHA** | • Umati mkubwa wa watu ulikuja kumsikiliza Yesu. Lilikuwa kusanyiko kubwa kwa hivyo Yesu alipanda mashua ikiwa baharini na kuketi ndani yake, wakati akiwafundisha watu waliokuwa nchi kavu. Aliwafundisha habari nyingine. ***(Marko 4: 1-2)*** *Jadili - kwa nini unafikiri kila mtu alitaka kusikiliza habari za Yesu? Unafikiri ungetaka kusikiliza habari zake kama ungeishi wakati huo?*<br>• Kulikuwa na mkulima aliyepanda mbegu kwenye udongo. Mbegu zilianguka kwenye aina nne tofauti za udongo. Baadhi yake zilianguka njiani na kuliwa na ndege kwa hivyo hazikuota kabisa. Zingine zilianguka kwenye udongo wa miamba. Hazikuweza kutengeneza mizizi mizuri kwa hivyo zikafa mara tu baada ya kuota. Zingine pia zilianguka kati ya miiba na miiba ikazisonga. Kulikuwa na mbegu zilizoanguka kwenye udongo mzuri. Zikatoa mazao mazuri. ***(Marko 4: 3-9)*** *Waambie watoto kwamba mbegu katika habari hii ni kama Neno la Mungu. Neno la Mungu ni Biblia. Eleza kwamba ikiwa tunataka kusikia Neno la Mungu tunapaswa kusoma Biblia.*<br>• Yesu aliendelea kuelezea mfano huo. Mbegu zinapoanguka njiani na ndege kuzila, ni kama wakati watu wanaposikia Neno la Mungu, kisha Shetani hulinyakua. Wakati mbegu inapoanguka kwenye udongo wa miamba ni kama wakati watu wanaposikia Neno la Mungu, na kumfuata Yesu lakini wanabadilisha mawazo yao mara tu nyakati ngumu zinapowapata. Wakati mbegu imesongwa na miiba ni kama watu wanaosikia Neno la Mungu lakini wanafikiria zaidi pesa zao na mali kuliko wanavyofanya kwa ajili ya Bwana Yesu. Wakati mbegu inapoanguka kwenye udongo mzuri ni kama watu wanaosikia neno la Mungu, wakalipokea na kukua hata kuwa Wakristo hodari. ***(Marko 4: 13-20)*** *Eleza kwamba Mungu anataka tuwe kama udongo mzuri na kuamini kile anachosema katika Neno lake yaani Biblia. Jadili - unafikiri tunawezaje kuwa kama udongo mzuri?*<br>• *Jadili - Je! Katika mifano tuliyojifunza ni mfano upi ambao umeupenda zaidi? Kwa nini umeupenda? Je! Ni somo gani muhimu zaidi ambalo umejifunza kutoka kwenye mfano huo?*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mpanzi<br><br>Unaweza kuonesha mbegu kama vile, punje ya ngano, pia shina la ngano ambalo liko tayari kuvunwa. Hii itasaidia kuonesha ukubwa wa mazao kama ilivyotajwa katika Mstari Muhimu. Mstari mbadala wa Daraja la 1 – ***Zaburi 119: 42*** kama somo la Wakati na Biblia. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Marko 4: 20***. Unaweza kutumia vitendo kuwasaidia watoto kukumbuka kila kifungu kama vile, kupanda = kutawanya, sikia = mkono uliozunguka sikio, kubali = elekeza mkono kwenye moyo, mmea kuzaa mazao = mikono kwa pamoja ikielekea juu. Nambari zinaweza kuandikwa hewani. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Yesu alikuwa wapi wakati akiwafundisha watu?<br>• Mkulima alifanya nini?<br>• Aina ya kwanza ya udongo ambapo mbegu ilianguka ilikuwa wapi?<br>• Aina ya pili ya udongo ilikuwaje?<br>• Aina ya tatu ya udongo ilikuwaje?<br>• Aina ya nne ya udongo ilikuwaje?<br>• Ni udongo upi ulikuwa bora zaidi kwa kupanda mazao?<br>• Je! Mbegu ikoje? |

## B6 Habari ya Kwanza
**Kijana Mwota ndoto - Habari hii inahusu ndoto za ajabu za Yusufu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Maisha katika familia ya Yusufu hayakuwa ya furaha wakati wote.<br>• Mungu alikuwa na mpango kwa ajili ya maisha ya Yusufu, na ana mpango kwa ajili ya maisha yetu pia.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 37: 8***<br>**Neno la Biblia:** ***Mwanzo 37: 1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Yusufu alikuwa na ndugu kumi na mmoja. Waambie watoto washirikishe taarifa kuhusu kaka na dada zao. Wana kaka na dada wangapi? Inafananaje kuwa mkubwa kuliko wote/kuwa wa katikati/kuwa mdogo kuliko wote katika familia?<br>Jadili ingekuwaje kukulia katika familia kubwa kama hii. |
| **FUNDISHA** | • Yakobo, baba yake Yusufu, aliishi katika nchi ya Kanaani. Yusufu alikuwa na umri wa miaka 17. Aliwasaidia ndugu zake kuchunga kondoo za baba yake. Siku moja aliwaona wakifanya jambo baya. Akamwambia baba yake kuhusu jambo hilo. ***(Mwanzo 37: 1-2)***<br>• Yakobo alimpenda Yusufu kuliko wanawe wengine kwa sababu alikuwa mtoto wa uzee wake. Israeli alimtengenezea Yusufu kanzu nzuri ya rangi nyingi. Ndugu za Yusufu walipoona hilo wakapata wivu sana. Wakamchukia! ***(Mwanzo 37: 3-4)*** *Jadili pamoja na watoto kuhusu neno 'wivu'. Je! Ina maana gani kuwa na wivu? Je! Umewahi kuwa na wivu? Unadhani kwanini ndugu walikuwa wakimwonea wivu Yusufu?*<br>• Yusufu aliota ndoto. Aliota kwamba yeye na kaka zake walikuwa wakifanya kazi mashambani na kufunga miganda ya mahindi. Mganda wa mahindi wa Yusufu ukasimama wima na miganda ya kaka zake ikauinamia.<br>• *Waeleze watoto kwamba ndoto hii ilikuwa na maana maalum kwa Yusufu juu ya kile kitakachomtokea baadaye. Waambie watoto wajadili kile wanachofikiria kwamba ndoto hiyo ilimaanisha. Ndugu zake walimchukia zaidi kwa sababu ya ndoto zake na maneno yake.* ***(Mwanzo 37: 5-8)***<br>• Yusufu aliota ndoto nyingine yenye maana inayofanana sana na hiyo ya kwanza. Wakati huu aliona jua, mwezi na nyota kumi na moja zikimsujudia. Sasa hata baba yake akamkasirikia. Akasema, Je! Mimi na mama yako na kaka zako tutakuja kukusujudia hata nchi? ***(Mwanzo 37: 9-10)***<br>• Kaka zake Yusufu walikuwa na wivu zaidi lakini baba yake aliendelea kufikiria juu ya hizi ndoto. ***(Mwanzo 37: 11)****.Waulize watoto kile wanachofikiria kitamtokea Yusufu baadaye. (Ndoto hizo zilimaanisha kwamba siku moja atawatawala ndugu zake.) Wakumbushe kwamba Mungu alikuwa na mpango kwa ajili ya maisha ya Yusufu tangu mwanzo. Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yetu pia.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kijana mwotaji. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mwanzo 37: 8***. Pengine sehemu ya kwanza kwa ajjili ya watoto wadogo. Eleza kwamba kaka za Yusufu walielewa maana ya ndoto zake. Walimuonea wivu na kumchukia. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Je! Yusufu alikuwa na umri gani katika habari hii?<br>• Je! Yakobo alimpa Yusufu zawadi gani?<br>• Kwa nini ndugu za Yusufu walimuonea wivu?<br>• Wivu ni nini?<br>• Je! Unafikiri ni sawa kuwa na wivu? (ndiyo au hapana)<br>• Yusufu aliota nini katika ndoto yake ya kwanza / ya pili?<br>• Ndoto za Yusufu zilimaanisha nini?<br>• Ni nani alipanga maisha ya Yusufu tangu mwanzo?<br><br>Kama mbadala, watoto wanaweza kutengeneza kolagi ya kanzu ya Yusufu. Kanzu ambayo imechorwa tu kwenye kipande cha karatasi inaweza kukatwa vipande 12. Kila kikundi kidogo cha watoto kina jukumu la **kuweka vikaratasi vya** rangi moja kwenye kipande cha kanzu walichopewa. Kanzu inaweza kuunganishwa tena ikikamilika. |

<u>**B6 Habari ya Pili**</u>

**Ndugu Aliyechukiwa - Habari hii inahusu Yusufu kuuzwa na kaka zake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yusufu aliuzwa na kaka zake utumwani.<br>• Hatuwezi kumficha Mungu dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Hesabu 32: 23***<br>**Neno la Biblia:** ***Mwanzo 37: 12-36*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto ikiwa wanafanya kazi za nyumbani au kuwafanyia wazazi kazi zingine kama vile Yusufu alivyofanya. Wakumbushe watoto habari iliyotangulia. Kwa nini ndugu za Yusufu walimchukia? Katika habari ya leo, Yusufu aliambiwa na baba yake aende kujua hali ya kaka zake ambao walikuwa mbali na nyumbani wakichunga kondoo zao. ***(Mwanzo 37: 12-17)*** |
| **FUNDISHA** | • Ndugu walimwona Yusufu akija. Walimchukia sana kiasi kwamba walipanga njama za kumuua. Tuone ndoto zake zitakuwaje. Wangeenda kusema uwongo na kumwambia baba yao kuwa mnyama wa porini alikuwa amemshambulia. ***(Mwanzo 37: 18-20)*** *Sema kwamba ndugu zake walifikiria wangeweza kuficha dhambi zao na kwamba kamwe hakuna mtu angegundua. Mungu anajua kuhusu mambo yote mabaya tunayofanya.*<br>• Reubeni, kaka mkubwa wa Yusufu, aliwazuia kufanya hili. Badala yake akawaambia wamtupe Yusufu ndani ya shimo. Alipanga kurudi baadaye na kumwokoa. ***(Mwanzo 37: 21-22)***<br>• Yusufu alipofika wakamvua kanzu yake yenye rangi nyingi na kumtupa kwenye shimo tupu lililokuwa halina maji. ***(Mwanzo 37: 23-24)***<br>• Muda mfupi baada ya kufanya hivyo, wanaume fulani wakapita. Walikuwa wamebeba viungo vya kuongeza ladha ya chakula kwenda kuviuza Misri. Ndugu mmoja, Yuda, alitaka kupata pesa. Badala ya kumuua Yusufu, yeye akapendekeza kwamba wamuuze Yusufu kwa wanaume hawa. Wakamuuza Yusufu kwa vipande 20 vya fedha. Yusufu alipelekwa Misri kufanya kazi kama mtumwa. ***(Mwanzo 37: 25-28)*** Mtumwa ni mtu gani? *Je! Unafikiri Yusufu alikuwa anajisikiaje sasa?*<br>• Ndugu zake Yusufu walijaribu kuficha kile walichokuwa wamefanya. Walichukua kanzu ya Yusufu na kuitumbukiza katika damu ya mbuzi. Wakairudisha kwa baba yao na kumuuliza kama ni ya Yusufu. Yakobo alitambua kanzu hiyo. Alifikiri mnyama mkali alikuwa amemshambulia Yusufu na kumuua. Yakobo alifadhaika sana na hakuweza kufarijika. ***(Mwanzo 37: 29-35)***<br>• Wakati huo, Yusufu alikuwa hai Misri. Alikuwa ameuzwa kwa mtu aliyeitwa Potifa ambaye alikuwa mkuu wa askari katika jeshi la Mfalme. ***(Mwanzo 37: 36)***<br>• *Wakumbushe watoto kuwa ingawa mambo yalionekana kuwa mabaya kwa Yusufu, Mungu aliendelea kuyasimamia yote.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ndugu aliyechukiwa |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Hesabu 32: 23***. Hakikisha kwamba watoto wanaelewa maana ya 'dhambi' na kwamba siku zote dhambi inastahili kuadhibiwa. Eleza kwamba Mungu anajua kuhusu dhambi zetu zote na dhambi zote lazima ziadhibiwe. Wakumbushe watoto kwamba Bwana Yesu alikufa msalabani kuchukua adhabu ya dhambi zetu. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Je! Yakobo alimwuliza Yusufu afanye nini mwanzoni mwa habari ya leo?<br>• Ndugu walipanga kumfanyia nini Yusufu?<br>• Ndugu yupi aliwaambia wasimuue Yusufu bali wamtupe ndani ya shimo badala ya kumuua?<br>• Yusufu aliuzwa kwa fedha ngapi?<br>• Ndugu walifichaje dhambi yao?<br>• Je! Yakobo alifikiri jambo gani lilimpata Yusufu?<br>• Nani alikuwa akitazama kwa ujumla kilichotokea katika maisha ya Yusufu?<br>• Mstari Muhimu unapatikana wapi? |

## B6 Habari ya Tatu

**Mfungwa Mwaminifu – Habari hii inahusu Yusufu kufungwa gerezani.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yusufu alikuwa mwaminifu na mchapakazi, hata gerezani.<br>• Mungu alikuwa pamoja na Yusufu. Hatatuacha kamwe wala kutuvunja moyo.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 39: 21***<br>**Neno la Biblia:** ***Mwanzo 39: 1-6 & 19-23*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto ikiwa wamewahi kuwa mbali na familia zao. Je! Hali hiyo iliwafanya wajisikieje? Kwa kifupi wakumbushe watoto jinsi ilivyomtokea Yusufu kuwa mbali na familia yake na jinsi alivyonunuliwa na Potifa kuwa mtumwa wake. Jaribu kuelezea jinsi ambavyo Yusufu alijisikia kuwa katika hali hii, kuwasili katika nchi tofauti na kuuzwa awe mtumwa. |
| **FUNDISHA** | • Yusufu alipelekwa Misri na kuuzwa kama mtumwa kwa mtu aliyeitwa Potifa. Potifa alikuwa akida katika jeshi la Mfalme. Potifa aliona kwamba Yusufu alikuwa mwaminifu na mchapakazi. Alijua kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na akamweka kuwa msimamizi wa kaya yake. ***(Mwanzo 39: 1-4).***<br>• Tangu Potifa alipomuweka Yusufu kuwa msimamizi wa nyumba yake, Mungu alibariki nyumba yake. Yusufu aliaminika kiasi kwamba Potifa alimpa mamlaka ya kufanya maamuzi. ***(Mwanzo 39: 5-6)****. Wasaidie watoto kuelewa baraka ni nini, kwa kueleza kwamba kibali cha Mungu kilikuwa juu ya nyumba ya Potifa kwa sababu ya Yusufu. Wakumbushe watoto kuwa Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na alikuwa akimtunza.*<br>• Siku moja, mke wa Potifa alimlaumu Yusufu kwa jambo ambalo hakufanya. Alimwambia Potifa uongo kumhusu Yusufu. Potifa alimwamini mkewe. Alikasirika sana na kumfanya Yusufu atupwe gerezani ingawa hakuwa amefanya chochote kibaya. ***(Mwanzo 39: 19-20)***. Eleza jinsi gani mabadiliko yalikuwa makubwa kwenye maisha ya Yusufu, yaani kutoka kwenye nyumba ya Potifa kwenda gerezani. *Je! Mungu alikuwa amesahau kuhusu Yusufu? Umewahi kulaumiwa kwa jambo ambalo hukufanya? Ulijisikiaje?*<br>• Lakini Mungu alikuwa bado yuko pamoja na Yusufu na alimtunza hata gerezani. Yusufu aliendelea kuwa mwaminifu na mchapakazi. Mlinzi wa gereza akamweka Yusufu kuwa msimamizi wa wafungwa wengine wote. Chochote alichofanya Yusufu gerezani, Mungu alikifanikisha. ***(Mwanzo 39: 21-23)***<br>• *Elezea kwa muhtasari sifa nzuri ambazo Yusufu alionesha katika sehemu hii ya habari. Ingekuwa rahisi kwa Yusufu kumpa kisogo Mungu lakini Yusufu aliendelea kumpendeza Mungu. Mungu alikuwa akimwandaa Yusufu kwa majukumu ambayo angekuwa nayo katika siku zijazo. Hakuwa amemsahau Yusufu na asingemwacha kamwe.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mtumwa mzuri / mfungwa mwaminifu |
| **JIFUNZE** | Fundisha na kuelezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mwanzo 39: 21 (sehemu a)***. Eleza watoto kwamba wakati mwingine mpango wa Mungu kwetu unaweza kujumuisha nyakati ngumu. Walakini Mungu anatupenda na yuko pamoja nasi hata wakati huo. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.<br>• Ni nchi gani Yusufu alipelekwa?<br>• Nani alimnunua Yusufu?<br>• Potifa alifanya kazi gani?<br>• Kwa nini Potifa alimweka Yusufu kuwa msimamizi wa nyumba yake?<br>• Kwa nini Yusufu alitupwa gerezani?<br>• Je! Yusufu alifanya kosa lolote?<br>• Ni nani alikuwa pamoja na Yusufu, na kufanikisha kila kitu alichofanya?<br>• Kwanini Mungu aliruhusu Yusufu kutiwa gerezani? |

## B6 Habari ya Nne

**Kiongozi Mpya – Habari hii inahusu Yusufu kuwa mtawala wa Misri.**

**Tunajifunza kuwa:**

- Yusufu akawa mkuu wa pili baada ya Farao katika nchi ya Misri.
- Mungu alikuwa amemuandaa Yusufu kwa kazi hii maalum.

**Mstari Muhimu:** ***1 Korintho 10: 13***
**Neno la Biblia:** ***Mwanzo 41: 14-49***

### TOA UTANGULIZI

Waulize watoto ikiwa wamewahi kuamka wakiwa wamepata ndoto ya kutatanisha. Je! Iliwafanya wajisikieje? Katika habari hii, Farao, Mfalme wa Misri, alikuwa na ndoto mbili ambazo hakuzielewa. Alitaka kujua zinamaanisha nini! Nani angeweza kumsaidia?

### FUNDISHA

- Farao alitaka kujua ndoto mbili za kutatanisha zilimaanisha nini. Katika ndoto yake ya kwanza aliota kwamba ng'ombe saba wanene walipanda katika Mto Nile. Kisha ng'ombe saba wembamba nao wakapanda. Ng'ombe wembamba wakawala ng'ombe walionona lakini wakawa bado wembamba kama hapo awali! Kisha akaota kuhusu masuke saba mazuri ya mahindi na masuke saba membamba ya mahindi. Masuke membamba yakameza masuke mazuri ya mahindi. Farao akawauliza wachawi wake waseme wanafikiri maana yake ni nini lakini hawakujua. ***(Mwanzo 41: 1-8)***
- *Waulize watoto wanafikiria ndoto hizo zinamaanisha nini. Mungu alikuwa amesababisha Farao kupata ndoto hizi. Yeye tu ndiye anayeweza kutoa jibu.*
- Farao akamuita Yusufu. Yusufu akatolewa gerezani na kuletwa kwa Farao. Waulize watoto wafikiri tukio hili lilikuwaje kwa Yusufu – jadili tofauti kati ya Gerezani na Ikulu. Alimwambia Farao kwamba hangeweza yeye mwenyewe kuzielezea ndoto, lakini Mungu atamsaidia kuelezea maana ya ndoto hizo. ***(Mwanzo 41: 14-24)*** *Wasaidie watoto kuelewa namna Yusufu alivyoweka tumaini lake kwa Mungu.*
- Mungu akamwambia Yusufu maana ya ndoto hizo. Yusufu akamwambia Farao maana yake. Ng'ombe saba walionona na masuke saba mazuri ya mahindi ilimaanisha kwamba hivi karibuni kutakuwa na miaka saba ya mavuno mazuri. Kila mtu atakuwa na chakula cha kutosha. Walakini, ng'ombe saba wembamba na masuke saba membamba ya mahindi vilimaanisha kwamba baada ya miaka saba ya shibe kutakuwa na miaka saba ya njaa. Njaa hiyo itakuwa mbaya sana kiasi kwamba kila mtu atasahau kuhusu miaka saba ya shibe. ***(Mwanzo 41: 25-32)****. Elezea janga la njaa ni nini, husianisha na matukio ya sasa kama inafaa.*
- Yusufu alipendekeza kwamba Farao achague wanaume wakusanye chakula wakati wa miaka ya shibe na kukihifadhi ili watu wale chakula hicho wakati wa miaka ya njaa. Wazo hili lilimpendeza Farao. Alijua kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na kwamba alikuwa mtu mwenye busara. Akamweka Yusufu kuwa msimamizi wa nchi yote ya Misri. Huko Misri, ni Farao tu ndiye alikuwa mkuu kuliko Yusufu. ***(Mwanzo 41: 33-45)***
- Wakati wa miaka ya shibe, Yusufu alitembea katika nchi yote ya Misri na kuhifadhi chakula kwa ajili ya miaka ya njaa. Kila mji ulikuwa na ghala la chakula kwa ajili ya njaa iliyokuwa bado haijatokea. Njaa ilipokuja watu walikuwa na chakula cha kutosha kula. ***(Mwanzo 41: 46-49)***
- *Wakumbushe watoto kuhusu maisha ya Yusufu hadi wakati huu. Jadili kuwa huu ulikuwa mpango wa Mungu kwa Yusufu katika kipindi chote hicho. Mungu alikuwa mwaminifu kwa Yusufu. Hiyo inamaanisha kwamba Mungu hakumuacha kamwe Yusufu lakini alikuwa huko kila wakati akitimiza makusudi yake katika maisha ya Yusufu. Alitumia nyakati zote ngumu katika maisha ya Yusufu kumtayarisha kwa jukumu hili muhimu. Mungu alimtumia Yusufu kuokoa maisha ya wengi wakati wa njaa!*

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**

**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kiongozi mpya

### JIFUNZE

Kama inafaa, fundisha na kuelezea, Mstari Muhimu. ***1 Wakorintho 10: 13*** - ***'Mungu ni mwaminifu'***. Jadili na watoto kuhusu maana ya 'mwaminifu' kama ilivyodokezwa hapo juu.

### KUMBUKA

Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kufanya marudio ya habari.

- Kwa nini Farao alimuita Yusufu?
- Ni nini kilichowapata ng'ombe katika ndoto ya kwanza?
- Ni nani alimsaidia Yusufu kuelezea maana ya zile ndoto?
- Ndoto hizo zilimaanisha nini?
- Kazi maalum ya Yusufu wakati wa miaka ya shibe ilikuwa nini?
- Je, ni jinsi gani Mungu alikuwa mwaminifu kwa Yusufu?

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**

- Kurasa nne kwenye kijitabu kina sehemu za kupaka rangi, kujaza maneno machache au kufanya kazi rahisi kila wiki.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**

- Kurasa 4 kila wiki kwenye vijitabu.
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari Muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**

Waalimu wanaombwa kwanza:

- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uziandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**

**Maoni ya jumla**

“Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.

“Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni.”

“Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho.”

**Maoni ya Kiroho**

“Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia.”

“Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena.”

**DARAJA LA PILI**

**Maoni ya jumla**

“Jibu zuri sana Wema!– “Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!”

“Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!”

“Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!”

**Maoni ya Kiroho**

“Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?”

“Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena.”

“Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu.”

## Kiambatisho A – Daraja la 0 & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B1** | **Maisha ya kwanza ya Kristo** | **Kutoa shukrani hekaluni** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-simeon-anna/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-simeon-anna/ |
| | | **Kukulia Nazareti** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-twelve/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-buildings/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-timothy/ |
| | | **Kujianda kwa ajili ya Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-baptised/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-john-baptist/ |
| | | **Yesu akutana na Yohana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-baptised/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-john-baptist/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-jesus-tempted/ |
| **B2** | **Miujiza** | **Yesu ageuza maji kuwa divai** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-jesus-wedding/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/wedding-cana-preschool/ |
| | | **Yesu aponya kijana mgonjwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-020-officials-son/ |
| | | **Yesu na Batimayo kipofu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-blind-bartimaeus/ |
| | | **Yesu awaponya watu kumi wenye ukoma** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-072-ten-leprosy/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-ten-leprosy/ |
| **B3** | **Bethania** | **Kujifunza kutoka kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-065-mary-martha/ |
| | | **Uzima kupitia kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-lazarus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-071-lazarus-resurrection/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-buildings/ |
| | | **Upendo kwa ajili ya Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mary-anoints-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-070-lazarus-dies/# |
| | | **Kumtazama Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-palm-sunday/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-king-jesus/ |

## Kiambatisho B – Daraja la 0 & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B4** | **Msalaba** | **Upendo wa Yesu/Kufa kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-easter/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-pontius-pilate/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-arrested/ |
| | | **Kufa kwa Yesu/Yesu afa na kuzikwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-easter/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-dies/ |
| | | **Yesu afufuka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-jesus-alive-2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-alive/ |
| | | **Kwenda na kurudi kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-alive/ |
| **B5** | **Mifano** | **Msamaria mwema** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-good-samaritan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rr-good-samaritan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-men2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-men1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-animals/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | **Kondoo aliyepotea** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-lost-sheep/ |
| | | **Mwana mpumbavu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-prodigal-son/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/prodigal-son-preschool/ |
| | | **Mpanzi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-parable-sower/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/parable-sower-preschool/ |
| **B6** | **Yusufu** | **Kijana mwotaji** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-dreamer/ |
| | | **Ndugu aliyechukiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-dreamer/ |
| | | **Mtumwa mzuri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-prison/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-kings-queens/ |
| | | **Kiongozi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-prison/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-brothers/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-kings-queens/ |

## Kiambatisho A – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| B1 | Maisha ya kwanza ya Kristo | **Mariamu na Yusufu Hekaluni** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/simeon-anna/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-010-simeon-anna/ |
| | | **Kukulia Nazareti** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-twelve/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-011-jesus-found/ |
| | | **Kubatizwa katika Mto Yordani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/john-baptist-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-013-jesus-baptism/ |
| | | **Kujaribiwa nyikani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-014-jesus-temptation/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-jesus-tempted/ |
| B2 | Miujiza | **Yesu ageuza maji kuwa divai** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-016-wedding-cana/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-wedding/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/wedding-cana/ |
| | | **Yesu aponya kijana mgonjwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-020-officials-son/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-centurion/ |
| | | **Yesu na kipofu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-blind-man/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-blindman-jericho/ |
| | | **Yesu awaponya watu kumi wenye ukoma** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-072-ten-leprosy/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-ten-leprosy/ |
| B3 | Bethania | **Kujifunza kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-065-mary-martha/ |
| | | **Uzima kupitia kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-lazarus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-070-lazarus-dies/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-071-lazarus-resurrection/ |
| | | **Upendo kwa ajili ya Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mary-anoints-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-070-lazarus-dies/ |
| | | **Kumtazama Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-jerusalem/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-078-triumphant-entry/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B4** | **Msalaba** | **Kufa kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-087-last-supper/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-089-prayer-garden/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-092-jesus-pilate/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-094-pilate/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-095-jesus-led/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-096-jesus-crucifixion/ |
| | | **Yesu afa na kuzikwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-099-jesus-burial/ |
| | | **Yesu afufuka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-101-jesus-resurrection/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-102-appearance-mary/ |
| | | **Kwenda na kurudi kwa Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-107-jesus-ascension/ |
| **B5** | **Mifano** | **Msamaria mwema** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rr-good-samaritan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/good-samaritan/# |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-good-samaritan/ |
| | | **Kondoo aliyepotea** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lost-sheep/ |
| | | **Mwana mpotevu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-067-prodigal-son/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-prodigal-son/ |
| | | **Mpanzi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-049-parable-sower/ |
| **B6** | **Yusufu** | **Kijana mwotaji** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yooseef-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/josephs-dreams/ |
| | | **Ndugu aliyechukiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-pit/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-slave/ |
| | | **Mfungwa mwaminifu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-potiphar/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-baker-cupbearer/ |
| | | **Kiongozi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-ruler/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/pharaoh-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers/ |

© Bible Educational Services 2020

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - 09/2023